# Nipashe

Jumatatu Agosti 31, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580324

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Wafugaji wadaiwa kuua mgambo, kujeruhi wanane

UKURASA 4




UKURASA 11

# Maalim Seif ahoji kura ya mapema

**ACHUKUA** fomu ya urais jana akisema...*Endelea ukurasa. 2*



Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Mkuu Mstaafu, Hamid Mahmoud Hamid, akimkabidhi fomu ya kugombea urais wa Zanzibar mgombea wa ACT- Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad Mjini Zanzibar, jana. **PICHA ZOTE RAHMA SULEIMAN**



Mgombea urais wa Zanzibar kupitia CCK, Othman Rashid Khamis, akipokea fomu ya kugombea nafasi hiyo kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Mkuu Mstaafu Hamid Mahmoud Hamid, Mjini Zanzibar jana.

## CHADEMA YABAINISHA VIPAUMBELE VYA ILANI



UKURASA 3


Nipashe

Fursa kwa Wagombea! 2020




**Gazeti la Nipashe**

**Linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini**

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

**Wasiliana nasi**
**Simu: 0686 101335,**
**Barua pepe: advertise@guardian.co.tz**


## CCM: Kibano rushwa pale pale miaka 5 ijayo

UKURASA 2

**MICHEZO** SOGNE WA YANGA KUTUA LEO NCHINI UK.23

MAONI, KATUNI UK.6



Baadhi ya wananchi wa Mtaa wa Engosowashi wakiwa katika mkutano wa uhamasishaji kwa ajili ya urasimishaji unaondelea kwenye mtaa huo uliopo Kata ya Moshono mkoani Arusha hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maalim Seif achukua fomu, ahoji kura ya mapema

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT- Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, jana amechukua fomu ya kugombea nafasi hiyo kupitia chama hicho na kuhoji sababu ya kufanyika upigaji kura ya mapema Oktoba 27, visiwani humo.

Alifika Ofisi za Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), majira ya saa 5:00 asubuhi na kukabidhiwa fomu hiyo na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Jaji Hamid Mahmoud.

Seif anakuwa mgombea wa 12 kuchukua fomu ya kugombea urais, huku mgombea wa 13 kutoka Chama cha CCK, Othman Rashid Khamis, naye alichukua fomu hizo ofisi za ZEC jana.

Akiwa ZEC mbele ya Mwenyekiti wa Uchaguzi, Maalim Seif alihoji kuhusu lengo la kufanyika kura ya mapema kwa kuwa watapiga tena kura Oktoba 28, mwaka huu kwa ajili ya Rais na wabunge wa muungano.

Akijibu swali hilo, Mwenyekiti wa Uchaguzi, Jaji Hamid Mahmoud, alisema kura ya mapema ipo kisheria, hivyo hakuna mjadala kura hiyo itakuwepo.

Akizungumza na wafuasi wa ACT-Wazalendo, katika ofisi za chama Vuga baada ya kurudi kuchukua fomu, Maalim Seif alisema hadi Tume ya Uchaguzi itakapomteua kuwa mgombea ndio ataeleza vipaumbele vyake kama atakuwa Rais wa Zanzibar.

Kadhalika, alisema anataka uchaguzi wa huru na haki na kwamba hawatakubali kuporwa ushindi kama ilivyokua kwenye uchaguzi uliopita.

Aliwataka viongozi wa dini kutohubiri amani pekee pia wahubiri haki kutendeka kwa kuwa bila mambo hayo kwenye uchaguzi mkuu amani haiwezi kupatikana.

Kwa mujibu wa Maalim Seif, alishangazwa kuona baadhi ya wagombea wa CCM wamepita bila ya kupigwa wakati wagombea wa vyama vingine wamechukua fomu wakiwamo wagombea wa ACT-Wazalendo.

"Hii ni dhahiri inaonyesha kuwa CCM wanaogopa uchaguzi hawawezi kupambana na hoja,"alisema Maalim Seif.

Alisema kuwa ACT-Wazalendo ipo tayari kushindana kwenye uchaguzi mkuu ili wananchi waweze kukipigia kura na kukipa ushindi.

Naye mgombea wa CCK, Othman Rashid Khamis, akizungumza baada ya kupokea fomu, alisema atahakikisha anailetea maendeleo Zanzibar na kulinda amani na utulivu wa nchi.

Alisema endapo atapata ridhaa za wananchi, atahakikisha anaboresha huduma muhimu za kijamii ikiwamo elimu na afya.

Wagombea 13 waliochukua fomu hadi jana ni Dk. Hussein Mwinyi kupitia CCM, Said Soud (AAFP), Juma Ali Khatib (Ada Tadea), Hamad Rashid (ADC), Mfaume Khamis (NLD), Ali Juma (Chauma), Issa Muhammed Zonga (SAU), Ameri Said Ameri (Demokrasia Makini) na Hamad Muhammed Ibrahim (UPDP).

Wengine ni Shafii Hassan Suleiman (Democratic Party), Khamis Faki Mgau (NRA), Maalim Seif Sharif Hamad (ACT- Wazalendo) na Othman Rashid Khamis (CCK).

# NEC yashughulikia pingamizi za ubunge

**Na Elizabeth Zaya**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema inaendelea kushughulikia rufani na pingamizi ziliyowekewa na wagombea wa vyama mbalimbali vya siasa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Mahera, alisema wanaendelea kufanya uchambuzi wa rufani na pingamizi hizo na kuwataka wananchi kuwa na subira.

Dk. Mahera alitoa kauli hiyo baada ya Nipashe kutaka kufahamu idadi ya pingamizi ambazo zimeshaamriwa mpaka sasa.

"Masuala ya pingamizi na rufani yamewekwa kotekote na ndiyo tunaendelea kuyashughulikia, haya ni mambo ya kisheria, muwe na subira," alisema Dk. Mahera.

Hivi karibuni, baadhi ya vyama hususani vya upinzani vimewalalamikia wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo 57 na kata 600 kuwaengua wagombea wao.

Aidha, wametaka haki kutendeka kwa kila chama kushindana kwenye sanduku la kura.

Juzi NEC ilitangaza majina ya wagombea 18 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), waliopita bila kupingwa na wanasubiri kukabidhiwa cheti cha ushindi wa ubunge mara baada ya uchaguzi kukamilika.

Akizungumza na waandishi wa habari Alhamisi ya wiki iliyopita, Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Bara, Benson Kigaila, alidai jumla ya wagombea wake 57 wa nafasi za ubunge na 600 wa udiwani walikuwa wameenguliwa.

Kigaila alitaja sababu ya wagombea wa chama hicho kuenguliwa kuwa ni pamoja na kutorudisha fomu za maadili, kutokuweka picha, wadhamini wa wagombea kutokuwapo kwenye orodha ya daftari la mpiga kura.

Nyingine ni majina ya wagombea katika kitambulisho chake kutofautiana na majina katika fomu aliyojaza ambazo alisema ni za kusingiziwa.

Chama kingine ambacho kinalalamika wagombea wake kuenguliwa ni ACT-Wazalendo.

# CCM: Kibano cha rushwa moto miaka mitano ijayo

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimejinasibu kuwa kitaendelea kudhibiti na kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa, uhujumu uchumi na ufisadi kwa miaka mitano ijayo.

Kwa mujibu wa ilani ya chama hicho kwa uchaguzi mkuu wa mwaka huu iliyosomwa na Katibu Mkuu wake, Dk. Bashiru Ally, wakati wa uzinduzi wa kampeni jijini Dodoma Jumamosi, baadaye kufafanuliwa na mgombea urais, Rais John Magufuli, kwamba fedha zitakazookolewa zitaelekezwa kwenye mipango ya maendeleo ya nchi.

Vilevile, chama hicho kimeeleza kuendelea kulinda na kuimarisha umoja, mshikamano, amani, utulivu, ulinzi na usalama wa nchi.

Mbali na hilo, sehemu ya Ilani hiyo inaeleza kuwa CCM katika miaka mitano ijayo imejipanga katika kudhibiti na kuimarisha mapambano dhidi ya uzalishaji, uingizaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya dawa za kulevya, utakatishaji wa fedha haramu na biashara ya kusafirisha binadamu.

Jukumu lingine ni kuendelea kulinda, kuimarisha na kudumisha uhuru, Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano wa Tanzania.

"Kuendelea kulinda na kuimarisha demokrasia ya vyama vingi, haki za binadamu, nchi isiyofungamana na dini yoyote na kupambana na unyanyasaji na udhalilishaji wa aina zote," ilieleza sehemu ya Ilani hiyo.

Mbali na jukumu hilo, Ilani hiyo pia ilieleza kuwa CCM itaendelea kuhakikisha Tanzania inakuwa nchi isiyofungamana na upande wowote, ili kutetea na kulinda maslahi ya nchi kwa kuzingatia misingi inayoiamini.

"Kuimarisha utumishi wa umma, unaozingatia weledi, nidhamu, uadilifu, bidii na maarifa katika kazi, kuimarisha mifumo ya kisera, kitaasisi na kisheria ikiwamo kutungwa kwa sheria inayotaka serikali za mitaa kutenga asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya uwezeshaji wa wanawake asilimia nne, vijana asilimia nne, watu wenye ulemavu asilimia mbili," inaeleza pia sehemu ya ilani hiyo.

Kadhalika, chama hicho kimeeleza kujikita zaidi katika kuimarisha uchumi wa viwanda, na kwamba mwaka 2015 kulikuwa na viwanda 52,633, lakini hadi kufikia mwaka jana idadi imeongezeka na kufikia 61,110, likiwa ni ongezeko la asilimia 16.1.

Ilani hiyo pia inaeleza kuwa CCM itatekeleza miradi ya mkakati yenye tija kubwa katika uchumi na ustawi wa jamii ikiwamo mradi wa kufufua umeme wa maji wa Julius Nyerere na ujenzi wa reli ya kisasa (SGR).

Mgombea urais wa CCM, Rais John Magufuli, akihutubia wananchi waliohudhuria uzinduzi wa kampeni wa chama hicho, alieleza kuwa ataendelea kusimamia amani, umoja na mshikamano uliopo nchini.

Alieleza kuwa pia ataendelea kukuza uchumi wa nchi kwa kuhakikisha unafikia asilimia nane, mfumuko wa bei kushuka pamoja na viwango vya riba katika benki kushuka.

Vilevile, aliahidi kuutokomeza umasikini na kuondoa tatizo la ukosekanaji wa ajira.

Kwenye sekta ya kilimo, Rais Magufuli aliahidi upatikanaji wa pembejeo, zana za kilimo pamoja na kuiboresha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania, kuipanua sekta ya umwagiliaji, kuimarisha huduma za ugani pamoja na vyama vya ushirika.

Kadhalika, aliahidi uhamasishaji na ufugaji wa kisasa, upatikanaji wa dawa na chanjo kwa ajili ya mifugo, ujenzi wa bandari ya uvuvi pamoja na kununua meli ya uvuvi.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii Dk. Aloyce Nzuki, akizungumza na wadau wa utalii wakati wa warsha ya kupokea maoni ya wadau wa utalii, iliolenga kurejesha utalii katika hali yake ya awali baada ya mapambano dhidi ya ugonjwa wa COVID- 19, iliyofanyika katika Chuo cha Taifa cha Utalii - Kampasi ya Arusha, jijini Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## ACT kukabidhi ilani wagombea wao

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kinatarajia kukabidhi ilani ya chama chake kwa wagombea wake wa nafasi ya urais wa Muungano kupitia chama hicho, Bernard Membe, pamoja na mgombea wake mwenza, Profesa Omar Fakih. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na chama hicho, tukio hilo litafanyika jijini Dar es Salaam.

"Kesho(leo) Agosti 31, Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, atakabidhi ilani kwa mgombea urais na mgombea wake mwenza, tukio hili litafanyika asubuhi saa 4:00,"ilieleza taarifa ya chama hicho.

Chama hicho bado hakijaweka bayana ratiba ya uzinduzi wa kampeni zake huku vyama vingine ikiwamo Chama Cha Mapinduzi (CCM), na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), vimeshazindua kampeni zake.

# CHADEMA yataja vipaumbele vyake

**Na Elizabeth Zaya**

MGOMBEA wa urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema moja ya vipaumbele vyake katika ilani ya chama hicho ni kuimarisha na kukuza sekta binafsi kuinua uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Akizungumza katika viwanja vya Tanganyika Parkers, Kawe, jijini Dar es Salaam ikiwa ni siku ya pili baada ya chama hicho kuzindua kampeni zake, Lissu alisema ilani ya chama hicho itajikita kwenye uhuru, haki, na maendeleo ya watu, na kwamba chochote ambacho watakisema kitasimamiwa na kaulimbiu hiyo.

Lissu alisema miongoni mwa mambo makubwa yatakayopewa nguvu katika serikali ya chama hicho ni pamoja na kujenga msingi wa uchumi huru utakaotokana na sekta binafsi.

Alisema serikali ya chama hicho itaweka msingi wa uchumi kwa kukaribisha sekta binafsi ndani na nje, kwa kuhakikisha inatengeneza mazingira mazuri ya kodi na taasisi.

Pia, alisema itajenga misingi mizuri ya usimamizi katika sekta hizo kwa kuhakikisha kwamba wanawajengea mazingira mazuri wawekezaji katika sekta ya viwanda pamoja na wafanyabishara katika sekta zote ya kutokuwa na hofu ya kunyang'anywa viwanda, biashara na pesa zao.

"Tukifanya hivyo, nchi hii itaneemeka kiuchumi kwa sababu pesa iko kwenye sekta binafsi, kwa hiyo lazima tutaipa ulinzi unaostahili ili pia isaidie kuajiri mamilioni ya vijana ambao hawana ajira, na serikali itakusanya kodi ambayo ni halali na kusimamia ustawi wa sekta hiyo," alisema Lissu.

Kadhalika, alisema endapo chama hicho kitafanikiwa kushika dola kitahakikisha kinashusha tozo ya mikopo ya elimu ya juu kutoka asilimia 15 ya sasa hadi kufikia asilimia tatu.

"Watakaotozwa kodi ni wale tu walio kwenye ajira," alisema.

Pia, alisema serikali yake itahakikisha inatengeneza mfumo wa elimu ambao utamsaidia kila anayefanikiwa kupata elimu hiyo inamsaidia kumpa maarifa ya kutatua matatizo pamoja na kupata ajira.

Kwa upande wake mgombea mwenza wa urais kupitia chama hicho, Salum Mwalimu, alisema endapo watafanikiwa kuingia madarakani, watafufua uhuru wa maendeleo katika kila sekta pamoja na uhusiano wa kimataifa.

"Wakati tunazunguka kutafuta wadhamini, tumekutana na changamoto za kijamii na kimaendeleo ambazo bado wananchi wanalia nazo, kwa hiyo sisi tutahakikisha kwamba tunazishughulikia," alisema Mwalimu.

**WABUNGE KUENGULIWA**

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Chama hicho, Freeman Mbowe, bila kutaja majimbo na majina, alisema wataendelea kupigania haki ya wagombea wao walioenguliwa mpaka wahakikishe haki inapatikana.

"Baadhi ya wagombea wetu wameachiwa, lakini wengine wameenguliwa, kwetu sisi jambo hili ni zito sana, tunapoona wagombea wanaenguliwa hatuwezi kufumbia macho," alisema Mbowe.

"Tume wasifikirie kwamba vyama vya upinzani vinapenda kulalamika isipokuwa tunachopenda ni haki kutendeka, tutaendelea kupigania haki za wagombea wetu."

**RELIANCE INSURANCE COMPANY (TANZANIA) LIMITED**

**TAARIFA KWA UMMA**

KAMPUNI YA BIMA YA **RELIANCE INSURANCE COMPANY (T) LIMITED** INAPENDA KUWATAARIFU WATEJA WAKE NA UMA KWA UJUMLA KWAMBA ***HAIWAKILISHWI TENA NA WAKALA WAKE*** **NALYCIA INSURANCE AGENCY** INAYOSIMAMIWA NA NDUGU **EMMANUEL DANIEL MWENGA YENYE OFISI ZAKE MBEYA, SUMBAWANGA, NJOMBE, KIBAHA, CHALINZE, DODOMA NA SONGEA.**

HIVYO BASI KAMPUNI YA RELIANCE INSURANCE COMPANY (T) LTD HAITAHUSIKA NA BIASHARA YOYOTE ITAKAYOFANYWA NA WAKALA HUYO KWA KUTUMIA JINA AU NYARAKA AU KWA NIABA YA KAMPUNI. PIA INAWAOMBA **WATEJA WOTE WALIOLIPIA BIMA KATI YA TAREHE 28/08/2019 HADI 27/08/2020** ***KWA KUPITIA WAKALA HUYO WAFIKE KWENYE OFISI YETU ILIYO KARIBU NAYE KWA MAELEZO MUHIMU.***

PIA INAOMBA KUWA YEYOTE ATAKEYEONA WAKALA HUYO AKIJIHUSISHA NA SHUHULI ZA BIMA KWA KUTUMIA JINA LA RELIANCE INSURANCE COMPANY (T) LTD AWASILIANE NASI KWA **NAMBA +255 222120088**

**THE CHIEF EXECUTIVE OFFICER**
**RELIANCE INSURANCE COMPANY (T) LTD**
**3RD8T4TH FLOOR, RELIANCE HOUSE, PLOT NO 356,**
**UN ROAD UPANGA**
**P.O.BOX 9826,**
**DAR ES SALAAM**
**TEL +255 222120088**
**TANZANIA**

215878302

## Bomu lilivyoua mtoto

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA.

MTOTO mwenye mwenye umri wa miaka tisa, mwanafunzi wa darasa la pili katika Shule ya Msingi Lemba katika Kijiji cha Kasumo Kata ya Kajana wilayani Buhigwe, Mkoa wa Kigoma, amepoteza maisha baada ya kulipukiwa na bomu

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, Kamishana Msaidizi wa Polisi James Manyama, alisema tukio hilo lilitokea Agosti 28, mwaka huu wakati mtoto huyo akiwa machungoni

Manyama alieleza mtoto huyo akiwa anachunga, aliokota bomu pasipo kufahamu na wakati akirejea nyumbani huku akilichezea lilimlipukia na kumjeruhi vibaya maeneo ya kichwa na tumboni kisha kupoteza maisha.

Vyombo vya usalama mkoani Kigoma vinaeleza huenda bomu hilo liliangushwa na makundi ya waasi kutoka Burundi ambayo yalikuwa yakitumia kijiji lilipotokea tukio hilo kama njia ya kwenda katika kambi ya wakimbizi ya Mtabila.

Alisema Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wataalamu wa vilipuzi kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) wamebaini bomu hilo lilikuwa la kutupwa kwa mkono.

Kufuatia tukio hilo, Jeshi la Polisi limewahimiza wazazi wananchi wanaoishi katika vijiji vya maeneo yanayopakana na Burundi kuongeza umakini pamoja na kuwaelekeza watoto wao kuacha kuokota vitu ili kuepusha madhara kama hayo yaliyotokea.

"Nitoe fursa hii kutoa wito kwa wazazi kuwaelekeza watoto wao pindi wanapoona vitu wasivyo vifahamu wasivichezee," alisema Kamanda huyo.

Baadhi ya vijiji vinavyopakana na Burundi ambavyo angalizo limetolewa kwao ni Kasumo, Nyamugari, Kibande, Migongo, Muyamana Kilelema.




Treni ya mizigo ikiwasili katika Stesheni ya Krokon jijini Arusha, ikiwa na Shehena ya Saruji Tani 320 kutoka Kampuni ya Tanga Cement ya jijini Tanga, hivi karibuni. Treni hiyo iliyokuwa na mabehewa nane ilipokelewa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Idd Kimanta, ikiwa sehemu ya safari ya majaribio kutoka Tanga kwenda Arusha. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wafugaji wadaiwa kuua mgambo, 8 wajeruhiwa

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

ASKARI wa Jeshi la akiba (mgambo) katika Kijiji cha Machema Kata ya Nampungu, wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma, Said Katimbe (46), ameuawa kwa kuchomwa mkuki kifuani na wanaodaiwa kuwa ni watu wa jamii ya kifugaji.

Katimbe anadaiwa kuchomwa mkuki mara mbili katika mapigano kati ya wafugaji na wakulima.

Aidha, katika tukio hilo watu wanane walijeruhiwa na wamelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru, baada ya kujeruhiwa na silaha za jadi zinazodaiwa kutumiwa na wafugaji.

Mtendaji wa Kijiji cha Machemba, Ally Sapanga, aliwataja waliojeruhiwa ni Zuberi Jafari, Mohammed Chikoko, Mohammed Lilundu, Jimu Mbandawe, Issa Saidi, Matumula Selemani, Zuberi Nasoro na Mohammed Sengani.

Alisema mapigano hayo yalizuka Agosti 28, mwaka huu, majira ya saa 11.30 jioni baada ya wafugaji hao kuvamia kijiji humo na kuwashushia kipigo watu waliokuwa katika sherehe za harusi bila kuuliza wa kupewa nafasi ya kujitetea.

Mtendaji huyo alibainisha kuwa kuna taarifa zinaeleza kuwa chanzo cha mapigano hayo ni wafugaji hao kuhisi kuwa wakazi wa Kijiji hicho kuiba mifugo yao iliyodaiwa kuwa ilipotea kwa kutoweka kwenye kambi zao.

Sepanga alisema wafugaji waliowashambulia kwa kutumia fimbo, sime, mikuki na mishale hali iliyosababisha taharuki na kuwafanya wananchi kukimbia kwa lengo la kujiokoa.

**KAULI YA POLISI**

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa alituma askari kutoka katika kituo cha polisi Tunduru kufuatilia na kuwatafuta wafugaji wanaodaiwa kufanya kitendo hicho.

Alisema kitendo cha wafugaji kuchukua sheria mikononi kimewaondolea haki yao kisheria hata kama walikuwa na hoja au madai ya msingi katika tukio hilo.

Aidha, Kamanda Maigwa aliwataka wananchi wenye taarifa za maeneo waliyokimbilia watuhumiwa hao kwa lengo la kijificha, kutoa taarifa Polisi ili wakamatwe na kupisha sheria kufuata mkondo wake.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wananchi waliiomba serikali kuwahamishia wafugaji hao katika maeneo ya vitalu vilivyotengwa kwa ajili ya shughuli za ufugaji.

Walidai kuwa wafugaji badala ya kuishi kwenye vitalu hivyo, wamevamia na kulisha mifugo yao kwenye makazi ya watu.

# Agizo la Mpina kashfa wizi wa ng'ombe 17 latekelezwa

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

AGIZO lililotolewa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, kuhusiana na kashfa ya wizi wa ng'ombe 17 wenye thamani ya Sh. milioni 14 katika Ranchi ya Taifa ya West Kilimanjaro limetekelezwa.

Utekelezaji huo umefanyika baada ya Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, kukabidhiwa ng'ombe hao baada waliokuwa watumishi wa ranchi hiyo kununua wengine.

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, alisema ng'ombe amekabidhiwa na Meneja wa Kampuni hiyo, Mbelwa Lutagwelera, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mpina aliyeagiza ngombe kurejeshwa kwenye ranchi na kukataa sababu zilizokuwa zimetolewa kuwa ng'ombe wameibiwa.

"Ni kweli nimepokea leo ng'ombe hao baada ya kurejeshwa kama Mh. Waziri alivyoagiza alipotembelea Ranchi hii kwamba mifugo hiyo ipatikane haraka na hatua ziendelee kuchukuliwa kwa wote waliohusika na kashfa hiyo," alisema Buswelu.

Pia Mkuu huyo wa wilaya ameagiza Menejimenti ya NARCO kuajiri walinzi wenye sifa na hasa waliopitia mafunzo kutoka kutoka Jeshi la Akiba ambao wamefundishwa uadilifu na uzalendo wa nchi yao, badala ya kuajiri watu wasiokuwa na sifa.

Buswelu aliwataka watumishi wa ranchi hiyo kusimamia ulinzi wa rasilimali za kampuni hiyo na kujiepusha na vitendo vya kuwa sehemu ya kuhujumu na kushiriki vitendo vya wizi na badala yake wazalishe ng'ombe wengi ili taifa lipate fedha nyingi kutokana na mifugo.

Wakati Waziri Mpina alipotembelea Ranchi hiyo, Mkuu wa wilaya hiyo aliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata kwa watumishi wote wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) West Kilimanjaro kufuatia kashfa ya kupotea kwenye mazingira ya kutatanisha ng'ombe 17 wa Serikali waliokuwa wanatunzwa kwenye ranchi hiyo.

Buselu amesema tangu wizi huo ufanywe hakuna taarifa yoyote iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya hiyo jambo linaoonesha kuna njama za makusudi zilizowekwa na watumishi hao kuiibia Serikali jambo ambalo halikubaliki.

Hivi karibuni, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, alipoitembelea wilaya hiyo, alieleza kutokuridhishwa na hatua zilizochukuliwa na uongozi wa Ranchi kuhusiana na kashfa hiyo na kuagiza kuwa ifikapo jumatano Julai 19, mwaka huu mifugo yote iliyopotea iwe imerejeshwa ndani ya Ranchi hiyo.

Waziri Mpina alisema hatua zilizochukuliwa za kuwasimamisha kazi watumishi wawili kufuatia wizi huo ni njama za kuficha mtandao wa uhalifu huo na kuagiza vyombo vya dola kufanya uchunguzi wa kina ili kuunasa mtandao wote uliohusika katika kashfa hiyo.

Akitoa taarifa kuhusu kampuni hiyo, Kaimu Meneja wa NARCO, Lutagwelera alisema kwa sasa wataendelea kushirikiana na Serikali ya wilaya hiyo katika kusimamia ulinzi wa rasilimali hizo ili vitendo kama hivyo visitokee tena ili kuongeza uzalishaji mifugo kwenye ranchi hiyo.

TANGAZO

# CHUO CHA USIMAMIZI WA FEDHA
# THE INSTITUTE OF FINANCE MANAGEMENT
*(ESTABLISHED UNDER THE ACT No. 3 OF 1972)*

THE INSTITUTE OF FINANCE MANAGEMENT
ESTD 1972
JIFUNZE UHUDUMIE

## *OFFICE OF THE DEPUTY RECTOR – ACADEMIC, RESEARCH & CONSULTANCY*

## APPLICATION FOR 2020/2021 ACADEMIC YEAR AT IFM DAR ES SALAAM CAMPUS, AND MWANZA TEACHING CENTRE

Applications are invited for admission (both direct entry and equivalent entry) at the Institute of Finance Management (IFM) for 2020/2021 academic year. The applications are open for the following programmes:

### A: APPLICATION FOR PROGRAMMES OFFERED AT IFM DAR ES SALAAM CAMPUS

| S/N | COURSE | DURATION |
|---|---|---|
| 1 | Bachelor of Accounting (BAcc) | Three years |
| 2 | Bachelor of Banking and Finance (BBF) | Three years |
| 3 | Bachelor of Science in Insurance and Risk Management (BSc IRM) | Three years |
| 4 | Bachelor of Science in Economics and Finance (BEF) | Three years |
| 5 | Bachelor of Science in Taxation (BSc Tax) | Three years |
| 6 | Bachelor of Science in Social Protection (BSc SP) | Three years |
| 7 | Bachelor of Science in Actuarial Science (BSc AS) | Three years |
| 8 | Bachelor of Computer Science (BCS) | Three years |
| 9 | Bachelor of Science in Information Technology (BSc IT) | Three years |
| 10 | Bachelor of Accounting with Information Technology (BAIT) | Three years |

### B: APPLICATION FOR PROGRAMMES OFFERED AT IFM MWANZA CAMPUS

| S/N | COURSE | DURATION |
|---|---|---|
| 1 | Bachelor of Accounting (BAcc) | Three years |
| 2 | Bachelor of Banking and Finance (BBF) | Three years |
| 3 | Bachelor of Science in Insurance and Risk Management (BSc IRM) | Three years |
| 4 | Bachelor of Science in Economics and Finance (BEF) | Three years |

### C: ENTRY REQUIREMENTS

**1.0 DIRECT ENTRY: (FORM SIX). Minimum point is 4 obtained in any two relevant subjects.**

| Bachelor Degree Programme | Specific entry requirements |
|---|---|
| Bachelor of Accounting (BAcc) | Two principal passes in the following subjects: Accountancy, Economics, Commerce, Physics, Chemistry, Biology, Advanced Mathematics, Geography, History, Kiswahili, English Language, Arabic, Agriculture, Computer Science. Those without a principal pass or a subsidiary pass in Advanced Mathematics or a pass in Basic Applied Mathematics must have a credit at O-Level |
| Bachelor of Banking and Finance (BBF) | Two principal passes in the following subjects: Accountancy, Economics, Commerce, Physics, Chemistry, Biology, Advanced Mathematics, Geography, History, Kiswahili, English Language, French, Arabic, Agriculture, or Computer Science. Those without a principal pass or a subsidiary pass in Advanced Mathematics or a pass in Basic Applied Mathematics must have a credit at O-Level |
| Bachelor of Science in Insurance and Risk Management (BSc IRM) | Two principal passes in the following subjects: Economics, Commerce, Accountancy, Physics, Chemistry, Biology, Advanced Mathematics, History, Geography, Kiswahili, English Language, French, Arabic, Fine Art, Agriculture, Computer Science or Nutrition. |
| Bachelor of Science in Economics and Finance (BEF) | Two principal passes in the following subjects: Economics, Commerce, Accountancy, Physics, Chemistry, Biology, Advanced Mathematics, Geography, Kiswahili, English Language, French, Arabic, Agriculture, or Computer Science. Those without a principal pass or subsidiary pass in Advanced Mathematics or Basic Applied Mathematics or Accountancy or Economics must have a credit at O-Level in Mathematics or Commerce |
| Bachelor of Science in Taxation (BSc Tax) | Two principal passes in the following subjects: Accountancy, Economics, Commerce, Physics, Chemistry, Biology, Advanced Mathematics, Geography, History, Kiswahili, English Language, French, Arabic, Agriculture, or Computer Science. Those without a principal pass or a subsidiary pass in Advanced Mathematics or a pass in Basic Applied Mathematics must have a credit at O-Level |
| Bachelor of Science in Social Protection (BSc SP) | Two principal passes in the following subjects: Economics, Commerce, Accountancy, Physics, Chemistry, Biology, Advanced Mathematics, History, Geography, Kiswahili, English Language, French, Arabic, Fine Art, Agriculture, Computer Science or Nutrition. |
| Bachelor of Science in Actuarial Science (BSc AS) | Two principal passes in Advanced Mathematics and Physics, Economics, Commerce, Accountancy, Chemistry, Biology, Agriculture, Computer Science, History, Geography, Kiswahili, English Language, French, or Arabic. |
| Bachelor of Computer Science (BCS) | Two principal passes in Physics and Advanced Mathematics |
| Bachelor of Science in Information Technology (BSc IT) | Two principal passes in the following subjects: Physics, Chemistry, Biology, or Advanced Mathematics. Those without a principal pass or a subsidiary pass in Advanced Mathematics or a pass in Basic Applied Mathematics must have a credit at O-Level. |
| Bachelor of Accounting with Information Technology (BAIT) | Two principal passes in the following subjects: Physics, Chemistry, Biology, Advanced Mathematics, Agriculture, Computer Science, Geography, Economics, Commerce, or Accountancy. Those without a principal pass or a subsidiary pass in Advanced Mathematics or a pass in Basic Applied Mathematics must have a credit at O-Level. |

**2.0 EQUIVALENT ENTRY: (DIPLOMA). All must have an average of "B" or GPA of 3.0, and at least four passes (excluding religious Subjects) at O' level.**

| Bachelor Degree Programme | Specific entry requirements |
|---|---|
| Bachelor of Accounting (BAcc) | Diploma in Accounting, Business Administration, Taxation, Customs and Tax Management, Financial Administration, Accounting, Banking and Finance, Government Accounting and Finance, or Public Sector Finance Management with an average of "B" or a minimum GPA of 3.0. |
| Bachelor of Banking and Finance (BBF) | Diploma in Accounting, Business Administration, Procurement and Supplies Management, Tax Administration, Public Sector Finance Management, Economics or Banking and Finance with an average of "B" or a minimum GPA of 3.0. |
| Bachelor of Science in Insurance and Risk Management (BSc IRM) | Diploma in Insurance and Risk Management, Social Protection, Tax Management Accounting, Banking and Finance, Business Administration or Economics with an average of "B" or a minimum GPA of 3.0. |
| Bachelor of Science in Economics and Finance (BEF) | Diploma in Tax Management, Accounting, Business Administration, Procurement and Supplies Management, Economics or Banking and Finance with an average of "B" or a minimum GPA of 3.0. |
| Bachelor of Science in Taxation (BSc Tax) | Diploma in Tax Management, Accounting, Business Administration, Procurement and Supplies Management, Economics or Banking and Finance with an average of "B" or a minimum GPA of 3.0. |
| Bachelor of Science in Social Protection (BSc SP) | Diploma in Social Protection, Accounting, Business Administration, Economics, Banking and Finance or Insurance and Risk Management with an average of "B" or a minimum GPA of 3.0. |
| Bachelor of Science in Actuarial Science (BSc AS) | Diploma in Actuarial Science, Computer Science, Software Engineering, Business Informatics, Computer Engineering, or Telecommunication Engineering Information Technology or Mathematics and Statistics with an average of "B" or a minimum GPA of 3.0. In addition, an applicant must have a minimum of "D" grade in Mathematics at O -Level. |
| Bachelor of Computer Science (BCS) | Diploma in Computer Science, Information Technology, Software Engineering, Business Informatics, Computer Engineering, or Telecommunication Engineering with an average of "B" or a minimum GPA of 3.0. |
| Bachelor of Science in Information Technology (BSc IT) | Diploma in Computer Science, Information Technology, Software Engineering, Business Informatics, Computer Engineering, or Telecommunication Engineering with an average of "B" or a minimum GPA of 3.0. |
| Bachelor of Accounting with Information Technology (BAIT) | Diploma in Accounting, Taxation, Customs and Tax Management, Financial Administration, Business Administration, Procurement and Supplies, Banking and Finance, ICT, Computer Science, Information Systems, Software Engineering, Business Informatics, Computer Engineering, Telecommunication Engineering, Business Administration, with an average of "B" or a minimum GPA of 3.0. |

### D: MODE OF APPLICATION

Candidates, who wish to apply for admission in any of the programmes listed, can do so using the online system through **http://www.ifmsis.ac.tz/oas**. This link is also accessible via the IFM website: http://www.ifm.ac.tz.

### E: APPLICATION FEES

The non-refundable application fee is TZS. 10,000/= only

### F: APPLICATION WINDOWS

The first-round of applications: 26th August to 25th September 2020.
The second-round of applications: 12th to 18th October 2020.

### G: CORRESPONDENCE ADDRESSES

For correspondence on admission, please use any of the following addresses:

**Admissions Office**
Institute of Finance Management,
5 Shaaban Robert Street,
P.O. Box 3918,
**11101 DAR ES SALAAM, TANZANIA.**
Phone: +255-22-2112931/3/4
Fax: +255-22-2112935
Mobile: +255-734-205 208, +255-734-205 029, +255-734 205 030
E-mail: registrar@ifm.ac.tz. Or admissions@ifm.ac.tz

**OR**

**IFM MWANZA TEACHING CENTRE**
Rocky City Mall, 3rd Floor Wing B,
Makongoro Road/ Furahisha Street, Plot 494 KV Kirumba
P. O. Box 2372, **MWANZA.**
Phone: +255-28-2501215/6
Mobile: +255-734-205026
E-mail: mtc@ifm.ac.tz.

**OR**

**IFM DODOMA TEACHING CENTRE**
P.O.BOX 1774, **DODOMA.**
Phone: +255-26-2323582
Mobile: +255-734-205025, +255-736-997773
E-mail: dtc@ifm.ac.tz.

**Warning:** It is an offence to submit false information when applying for admission. Applicants who will be discovered to have submitted a forged certificate or any other false information will not be considered for admission, and appropriate legal action will be taken against them.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Timu zimeweekeza waamuzi tendeni haki Ligi Kuu Bara

**PAZIA** Ligi Kuu Bara limefunguliwa rasmi jana kwa mechi ya Ngao ya Jamii kati ya Simba na Namungo FC kupigwa katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Kuchezwa kwa mechi hiyo, inamaana sasa Ligi Kuu Bara itaanza rasmi Jumapili ijayo katika viwanja tofauti nchini.

Tayari tumeona namna timu zote zilivyokuwa 'bize' kuimarisha vikosi vyao katika dirisha la usajili ambalo lilifunguliwa tangu Agosti Mosi, mwaka huu na likitarajiwa kufungwa leo saa sita usiku.

Zipo timu zilizolazimika kutumia kiasi kikubwa cha fedha kwenda nje ya nchi na kusajili wachezaji kwa gharama kubwa lengo likiwa kutoa ushindani wa kweli kwenye mbio za ubingwa. Lakini pia, tumeshuhudia hata zilizosajili wachezaji wa ndani zikitumia gharama kubwa kuwasajili nyota hao.

Hilo halikufanyika kwa kusajili wachezaji pekee bali pia baadhi ya klabu zimetumia gharama kubwa kuboresha mabenchi yao ya ufundi kwa kuajiri makocha kutoka ndani na nje ya nchi.

Kwa maandalizi hayo yaliyofanywa, ni wazi msimu huu ushindani utaongezeka zaidi na mashabiki wa soka wanatarajia kupata burudani ya kutosha.

Hata hivyo, tunafahamu kuna changamoto nyingi katika soka letu ambazo huchangia wachezaji na hata mashabiki kutofurahia soka letu.

Moja ya changamoto kubwa ni ubovu wa viwanja, suala ambalo Bodi ya Ligi nchini (TPLB) imekuwa ikilivalia njuga kila mara kwa kuvifungia vilivyo vibovu.

Lakini changamoto kubwa hususan msimu uliyopita imekuwa ni waamuzi kuzifinyanga sheria 17 za soka jambo ambalo limekuwa lizorotesha soka letu kupiga hatua.

Na si kuzotesha tu, bali pia huchangia kutopatikana kwa bingwa halali huku timu zingine zikishuka daraja kutokana na kuchangiwa na kuvurunda kwa waamuzi.

Hivyo, wakati huu timu zikiendelea kufanya maandalizi ya mwisho, tunatarajia pia Chama cha Waamuzi nchini (FRAT), kitakuwa kimewapiga msasa marefa kwa kukumbushana sheria 17 za soka.

Tunasema hivyo, kwa sababu tunajua kwamba Waamuzi ndio wanaoshikilia 'roho' ya mchezo wa soka, kwani kuboronga kwao kunafanya kupatikana kwa bingwa ambaye si halali.

Pia waamuzi ndio ambao wanaweza kudumaza soka la Tanzania kwa kuziwezesha timu kupata matokeo mazuri na ya kuvutia, wakati uwezo wao ni mdogo na hivyo kuchangia kuzorotesha sekta hiyo.

Hivyo, Nipashe inawakumbusha na kuwaasa waamuzi wote wa soka, kuhakikisha wanachezesha soka kwa haki na kwa kuzingatia sheria na kanuni ili mwisho wa siku bingwa apatikane kihalali.

Pia Nipashe tunaamini kwa usajili mkubwa uliofanywa na baadhi ya klabu kwa kuleta nyota wa viwango vya juu kutoka nje ya nchi, kutazidi kuwavutia mashabiki wengi kutoka nje kufuatilia Ligi Kuu Bara.

Kwa mantiki hiyo, ni wakati wa waamuzi kurekebisha makosa yao kwa kufuata sheria 17 za soka hatua ambayo pia itawafanya kuaminika na kupangwa kuchezesha mechi kubwa za kimataifa za Fifa na CAF.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mbwebwe za usajili zimeisha, sasa uwanjani tu

**KWA** muda wa mwezi mmoja sasa tumeshuhudia mbwembwe za usajili kwa klabu mbalimbali ambazo zilikuwa zikileta wachezaji kwa ajili kuimarisha vikosi vyao kwa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2020/21.

Kuna waliokuwa wanajitambulisha kwenye mitandao ya kijamii, waliwapata wanachama na mashabiki wao kununua mabando kwa ajili ya kuingia kwenye akaunti zao ili kujua nani amesajiliwa.

Kuna klabu zilikuwa zikiwataka wanachama na mashabiki wao kwenda Uwanja wa Ndege kupokea wachezaji. Hizi zote zilikuwa ni mbwembwe za usajili, ambazo zilichukua nafasi yake na kuwachemsha sana mashabiki wa soka mara baada ya ligi kumalizika.

Sasa hizo zote zimeisha. Jumamosi ijayo Ligi Kuu Tanzania Bara inaanza. Isije ikachukuliwa kuwa mbwembwe zote tulizoziona za usajili ndizo zitaakisi kile kilichoonekana kwenye usajili.

Usajili ni kitu kingine. Mbwembwe za kupokea na kutambulisha kwenye mitandao ni kitu kingine, na kucheza uwanjani nacho ni kitu kingine.

Siasa za usajili zimemalizika, hivi sasa wanaachiwa mabenchi ya ufundi kufanya kazi yao ili kile kilichoaminishwa kwa wanachama na mashabiki kionekane uwanjani.

Ni wakati sasa wa viongozi na mabenchi ya ufundi kutulia na kutengeneza timu yenye ushindani.

Uwanjani hakuna mbwembwe, ni kile tu ambacho kilifanyika mwanzo kitaalam na kwenye benchi la ufundi.

Tunaweza kuona klabu ambazo hazikusajili kwa makeke, wala kuonyesha kwenye mitandao ya kijamii, wala kuongozana kumpokea Uwanja wa Ndege timu zake zikifanya vizuri na kuzitetemesha zile ambazo zilidhani kuwa zimesajili vizuri.

Angalizo langu ni kwamba isije kuwa timu zisizokuwa na makeke zikafanya vizuri, halafu zile ambazo zilidhani zimesajili vizuri zikaanza kugeuza kibao na kuanza kulalamikia waamuzi.

Kwenye soka la Tanzania kuna mambo mengi, lakini pia kuna siasa nyingi.

Klabu kubwa kama za Simba na Yanga zinaweza kujisifu kuwa zimesajili majembe ambayo kwenye ligi hii hakuna wa kuyasimamisha, lakini zikianza kusimamishwa na kupelekwa mchakamchaka, hawaamini kuwa wenzao nao walisajili vizuri, bali wanaamini kuwa waamuzi hawawatendei haki.

Ni kweli baadhi ya waamuzi Tanzania wana matatizo sana. Tuliona hata msimu uliopita jinsi walivyovurunda baadhi ya mechi, lakini si mechi zote kwa sababu hizo hizo Simba na Yanga nazo kuna baadhi ya mechi zimeonekana kubebwa pia.

Sasa kimefika kipindi cha kuangalia timu gani imesajili kikosi kizuri, timu gani imeongeza wachezaji wenye tija na timu gani ina kikosi kipana na mengine yanayofanana na hayo.

Kipindi cha siasa za usajili na maneno maneno kimekwisha, sasa ni miguu ya wachezaji tu ndiyo itaongea kuanzia Jumamosi ijayo.

Hatutarajii lawama zisizo za msingi kwa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), Bodi ya Ligi, wala waamuzi, kwani klabu zote zinaamini kuwa zimesajili wachezaji wazuri na wenye uwezo mkubwa.

Kwa maana hiyo, timu iishinda ishinde na kufurahia, lakini ikifunga basi ikubali kuwa imezidiwa na si kila kukicha lawama sizizokuwa na msingi.

Isije tu ikaonekana kwa sababu kuna baadhi ya timu zimesajili vizuri, basi hazina haki ya kushindwa, au haziwezi kufungwa.

Tumeona hata msimu uliopita, Simba pamoja na kuwa na kikosi bora na kuzidi timu za Ligi Kuu kwa pointi nyingi, lakini ilifungwa na Mwadui na Mbao FC ambazo zilicheza ligi hiyo zikiwa hoi bi taaban. Mbao FC imeshuka daraja, huku Mwadui ikiponea chupuchupu.

Pia, isidhaniwe kuwa timu yenye wachezaji bora, wenye majina makubwa, au walionunuliwa kwa gharama kubwa ndiyo itakuwa ikishinda tu, au kupata ubingwa, siyo kweli.

Timu itakayoshinda ni ile itakayokuwa imejipanga kwenye mechi husika, na itakayochukua ubingwa ni ile itakayokuwa na kikosi kipana, chenye wachezaji wanaolingana uwezo na benchi bora la ufundi.

Nizitakie kila la kheri timu zote 18 zitazoanza safari ya kuusaka ubingwa na kuwakumbusha tena kuwa mbwembwe za usajili zimekwisha, sasa mambo yako uwanjani.

# KKKT yajiweka kando na vyama vya siasa

**Na Elisante John,** SINGIDA

ASKOFU Msaidizi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kati Singida, Mchungaji Dk. Cyprian Hilinti, ameahidi kanisa hilo kutojihusisha na chama chochote cha siasa kwa nia ya kukiunga mkono.

Hata hivyo, amesema nafasi iko wazi ya kufanyiwa maombi mgombea aliyeahidi kulisha ubwawa wanafunzi, iwapo atapata ridhaa ya kuiongoza Tanzania.

Akizungumza jana kwenye ibada katika Usharika wa Imanuel, maarufu 'Kanisa la Msalaba mrefu', kabla ya muumini wa kanisa hilo anayewania pia ubunge Jimbo la Singida Mjini kupitia CHADEMA, Rehema Mkoha, ambaye alikua anatoa shukrani ya pekee, Mchungaji Dk. Hilinti, alifafanua kuwa kanisa hilo halifungamani wala kuunga mkono chama chochote cha siasa.

Mgombea ubunge huyo alikuwa anamtolea Mungu shukurani ya pekee, baada ya kupitishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) awe mgombea wa nafasi hiyo. Mchungaji Dk. Hilinti alifafanua kuwa kwa muundo wa kanisa hilo, halifungamani wala kuunga mkono chama chochote cha siasa, lakini waumini wake ni wanachama wa vyama mbalimbali vya kisiasa, hivyo wanastahili kupatiwa huduma za kiroho ili kuimarisha imani zao.

"Sisi hapa kanisa letu halifungamani na chama chochote cha siasa. Hivyo hatuombei vyama isipokuwa tunaombea waumini wetu, ambao wamejiunga kwenye vyama vya siasa...aliyesema akishinda urais atatoa wali, akihitaji kuombewa aje tupo tayari kumwombea," alisema.

Aidha,Dk. Hilinti aliwaomba waumini wa kanisa hilo waendelee kumwomba na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa maombi na bila kuchoka kutokana na kulinusuru Taifa na janga la ugonjwa wa COVID-19.

Mchungaji Dk. Hillinti alisema kuna nchi nyingi duniani tena zenye nguvu kubwa kiuchumi zilibanwa na tatizo la ugonjwa huo na kulazimika kufunga mipaka yake, lakini Tanzania iliendelea kuchapa kazi, hivyo kuendelea kuimarisha uchumi wake.

Akizungumza baada ya kutoa shukrani ya pekee, mgombea ubunge Rehema, alisema kuwa aliona vema kumtolea Mungu shukrani hiyo kwa kumwezesha kuteuliwa na CHADEMA, nafasi hiyo.

"Unapojitosa katika nafasi kubwa kama hii na baadae ukaaminiwa na chama chako kwa kuteuliwa, unakuwa upo tayari kuelekea katika ubunge... sasa kilichobaki ni mhusika kutangaza sera na ilani ya uchaguzi ya chama ili wananchi wakuelewe,",alisema.




Kaimu Mkuu wa Huduma za Kifedha wa Tigo Pesa, Angelica Pesha, akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuingia makubaliano na kampuni ya usafirishaji ya Vigor Group ambayo inamiliki boti za ZanFast Ferries, ili kuwawezesha wateja wake kununua tiketi kwa njia ya Tigo Pesa. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Vigor Group, Toufiq Turky.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TIC: Milango ipo wazi kwa wawekezaji nchini

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

KATIKA kuhakikisha azma ya Serikali ya kuendeleza na kukuza uchumi wa viwanda, Kituo cha Uwekezaji Tanzania-TIC, kimesema ipo haja kwa wawekezaji kukitumia kituo hicho katika kufanikisha shughuli zao ambazo ndio chachu ya ukuaji wa uchumi huo.

Kituo hicho ambacho kinaratibu, kuhamasisha na kusimamia uwekezaji nchini sasa kinafanya jitihada za kuwatembelea wawekezaji kwenye maeneo ya uwekezaji wao ili kukagua na kutatua changamoto zinazowakabili.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo hicho , Maduhu Kazi, aliwatembelea wawekezaji mkoani Mtwara ambapo akiwa katika kiwanda cha Saruji cha Dangote, alisema lengo ni kuangalia kwa namna gani wanaweza kushirikiana na wawekezaji pamoja na wadau wa sekta mbalimbali za Serikali na binafsi zinazohusika na uwekezaji katika kufanikisha shughuli hizo nchini. "Nawapongeza sana wawekezaji wa kiwanda hiki cha Dangote, mnafanya kazi nzuri katika uwekezaji wenu, sisi TIC tupo kwa ajili yenu, kitumieni kituo hiki kwa maendeleo ya uwekezaji katika nchi yetu na sisi tupo tayari kuwahudumia wawekezaji wote ili kukidhi matarajio ya nchi katika ukuaji wa uchumi" alisema Dk. Kazi.

Meneja Mkuu wa Kiwanda cha Saruji cha Dangote, Aboyomi Awofodu, alisema kwa sasa kiwanda hicho kinafunga mitambo ya kisasa itakayowezesha kutumia umeme wa gesi, makaa ya mawe na maji ili kuwa na umeme wa uhakika wakati wote. Kiwanda cha Saruji cha Dangote chenye eneo la ekari 1,700 kilichopo katika eneo la Msijute katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara ni moja ya uwekezaji Mkubwa nchini.

Kiwanda hiki kilianza kazi Desemba 2015 na hadi sasa kinazalisha saruji ya kiwango cha daraja la 32.5 na 42.5 ambayo inatumika nchini na nyingine kusafirishwa nje ya nchi

# Msitu wa Minyughe Ikungi hatarini kupotea

**Na Dotto Mwaibale,** SINGIDA

HALI ya Msitu wa Minyughe uliopo Wilaya ya Ikungi mkoani Singida imeendelea kuwa mbaya kutokana na wakazi wanaouzunguka kuuvamia kwa kukata miti ovyo na kuingiza mifugo bila ya kufuata taratibu.

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya hiyo mwishoni mwa wiki ilitembelea na kujionea hali halisi na namna uvunaji wa mazao ya msitu huo ikiwemo ukataji wa miti na uchomaji wa mkaa ukifanyika bila ya kufuata utaratibu wimbi kubwa la wahamiaji kutoka mikoa ya jirani wakihusishwa na uharibifu huo.

Msitu huo wenye ukubwa wa takribani hekta 230,000 upo katika Tarafa za Sepuka, Ihanja na Ikungi na kuundwa na vijiji 26 wilayani Ikungi.

Msitu huo ulianzishwa chini ya mradi wa LAMP (Land Management Programme) ukifadhiliwa na Shirika la Sida la Uswisi mwaka 2002.

Msitu huo una uoto wa asili wa miti jamii ya miombo na maeneo kidogo ya mbuga na uoto adimu wa vichaka vya Itigi (Itigi Thickets) huku ukiwa na wanyamapori na viumbe wengine wa aina mbalimbali ambao walifanya makazi ndani ya msitu huo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa wilaya hiyo ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya, Edward Mpogolo akizungumza na wajumbe wa kamati hiyo, viongozi wa Kata ya Mwaru pamoja na waandishi wa habari wakati akikagua msitu huo, alisema lengo la kuuanzisha ilikuwa ni kutunza uoto wa asili na bioanuwai zilizokuwa hatarini kutoweka ikiwamo wanyamapori

Alitaja lengo lingine kuwa ni kutunza mazingira kwa ujumla na kupambana na hali ya kuenea kwa jangwa, kutunza rasilimali asili kwa kizazi kilichopo na kijacho pamoja na jamii kunufaika moja kwa moja na rasilimali misitu zilizopo.

Mpogolo alisema msitu huo ni nguzo ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi ukiungana na msitu wa mikoa ya Tabora, Rukwa na Katavi katika kuimarisha mvua zitokazo misitu ya Kongo.

"Msitu huu ni chanzo cha maji ya Ruaha Mkuu ( Internal Drainage) ukiunga pori la akiba la Rungwa, Muhesi na Kizigo lililopo Manyoni" alisema Mpogolo.

Alisema msitu huo ni kidaka maji ( Catchment Forest) kwa bonde la Wembere linaloweka uhai wa Ziwa Kitangiri na Eyasi.

Mpogolo alikamilisha kuzungumza na wajumbe hao na waandishi wa habari kwa kutoa maagizo ya kuwachukulia hatua watu wote waliovamia msitu huo kwa kujenga na kuingiza mifugo yao ambapo alitaka orodha yao ikiwa na kuondoka mara moja ndani ya msitu ndipo wafanye utaratibu wa kuomba upya kwa serikali ya kijiji.

"Haiwezekani kuingia kwenye hifadhi bila ya kufuata taratibu na kufanya uharibifu huu mkubwa, Serikali ya kijiji na kamati yangu ya ulinzi na usalama ni lazima tuhakikishe uhalibifu huu wa msitu haujirudii tena," alisema Mpogolo.

Alisema hali hiyo ikiachwa eneo hilo litakuwa jangwa na jamii inayoishi humo itapata matatizo ya maisha kwani hata madawa yatokanayo na miti ya asili hayatapatikana.

Mpogolo aliwaagiza viongozi wa halmashauri ya kijiji katika eneo hilo kuitisha mkutano utakaowakutanisha wavamizi hao na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo ili kujua walipataje kibali cha kuingia kwenye hifadhi hiyo kwani yamekuwapo madai ya watu kuwa kuna baadhi ya viongozi wasio waaminifu wa vijiji vinavyozunguka msitu huo kuchukua fedha au ng'ombe kutoka kwa wafugaji hao na kuwagawia ardhi katika hifadhi.

Alisema kupitia mkutano huo watawabaini viongozi waliojihusisha kwa namna moja au nyingine kutoa maeneo kwenye hifadhi hiyo nao watachukuliwa hatua za kisheria huku wavamizi hao wakifanyiwa utaratibu na halmashauri wa kutafutiwa maeneo mengine ya kuishi na kufanya shughuli za kilimo na ufugaji nje ya hifadhi.

Aidha Mpogolo alisema mvamizi atakayekaidi hatua hizo za awali za mazungumzo na kuwasikiliza atachukuliwa hatua kali ikiwamo kuondolewa kwa nguvu ndani ya hifadhi hiyo.

# Waomba suluhu mgogoro na TFS

**Na Ibrahim Yassin,** ILEJE

WAKAZI wa vijiji Vya Itale Ilomba na Ndola wilayani Ileje, mkoani Songwe, wameiomba Serikali kutatua mgogogoro wa ardhi kati yao na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ili kukwepa machafuko yasiyokuwa na tija yanayoweza kujitokeza.

Awali wananchi hao walizuiliwa kuendelea kufanya shughuli Katika maeneo hayo ambayo yanadaiwa kuwa ni mali ya TFS ambao wamekuwa wakiwapiga marufuku wananchi wa vijiji hivyo kufanya shughuli au kuokota kuni katika maeneo hayo.

Akizungumza mwishoni mwa wiki na gazeti hili, Isega Mwasenga, alisema eneo hilo la msitu ni mali ya kijiji na wao wana haki ya kuutumia msitu huo kwa matumizi mbalimbali lakini anashangaa kuona wanakatazwa kufanya shughuli katika msitu huo.

Naye Jack Mwahalenda, mkazi wa kijiji hicho, alisema wamekuwa hawana uhuru wa kuitumia misitu iliyopo katika vijiji vyao kwani kila msitu wakijalibu kuokota kuni kwa ajili ya matumizi ya kupikia wanakamatwa na kudaiwa hawana haki kwa kuwa misiti ni mali ya TFS.

Alisema kutokana na katazo hilo,wamekuwa hawana haki na kujiona kama si raia wa Tanzania kutokana na makatazo hayo, na kwamba wakazi wengi ni masikini hawana uwezo wa kutumia mkaa pamoja na majiko ya gesi, hivyo wanalazimika kuokota kuni katika misitu kwa ajili ya kupikia lakini wanakiona cha mtema kuni.

"Tunaomba serikali iingilie kati suala hili hili kuhepuka mapigano kati yao na maofisa wa misitu TFS yanayoweza kujitokeza kwani wamefikia hatua wanajenga uhasama na maafisa hao kutokana na katazo la kufanya shughuli katika misitu ikiwamo kuokota kuni," alisema Mwahalenda.

Meneja wa TFS Wilaya ya Ileje, Deogratus Kavishe, alisema wakala huo hauchukui maeneo mapya kwa sasa, na kuwa maeneo yao yalishapimwa na wataalamu tangu mwaka 1987 na wanayo ramani na vipimo za hifadhi hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Joseph Mkude, aliwataka wananchi hao kuendelea na shughuli zao isipokuwa hawatoruhusiwa kulima mazao ya muda mrefu kwa sasa, kwani eneo hilo lipo chini ya TFS, lengo kuu ni kulinda uharibifu wa mazingira.

000000

# Madaktari JKCI wafanya upasuaji mpya

**Na Joseph Mwendapole**

MADAKTARI bingwa wa upasuaji wa moyo, mishipa ya damu na kifua wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) kwa mara ya kwanza wamefanya upasuaji wa kupandikiza mishipa ya damu kutoka kwenye mshipa wa damu wa kifuani na kupeleka kwenye mishipa ya damu ya miguuni.

Upasuaji huo ni wa kwanza kufanyika hapa nchini ambapo mgonjwa alikuwa na tatizo la kupata maumivu makali maeneo ya miguuni, mapajani na sehemu ya kukalia kwa muda wa miezi nane.

Baada ya uchunguzi iligundulika kwamba mshipa wake mkubwa wa damu umeziba kabisa na hivyo kushindwa kupeleka damu kwenye miguu na damu ilikuwa inapelekwa kupitia mishipa midogo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, daktari bingwa wa upasuaji wa moyo, mishipa ya damu na kifua wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Alex Joseph, alisema walimpokea mgonjwa huyo wiki iliyopita kutoka Hospitali ya Mnazi mmoja iliyopo Visiwani Zanzibar.

Dk. Alex alisema upasuaji wa aina hiyo haujawahi kufanyika nchini hivyo baada ya majadiliano ya jopo la madaktari bingwa na kushauriana na mgonjwa waliona waufanye kwani kulikuwa na uwezekano mkubwa kwa mgonjwa kupona na kutoka katika maumivu makali aliyokuwa nayo. "Upasuaji tulioufanya ni wa kupandikiza mrija bandia wa damu na kuukwepesha eneo ambalo limeziba. Tuliweka mrija kama mshipa bandia wa damu kutoka kwenye mshipa wa damu wa kifua upande wa kushoto na kuupitisha pembeni ya kifua na tumbo mpaka kwenye mguu wa kushoto na kisha kuelekea mguu wa kulia", alisema.

"Baada ya kufanya upasuaji huo hivi sasa miguu yote miwili inapata damu ambayo inatoka moja kwa moja kwenye mshipa wa damu wa kifuani kwani tuliikwepesha eneo la tumboni ambalo mshipa umeziba," alisema Dk. Alex.

Dk. Alex alisema hii ni faraja kwao kwani hivi sasa huduma za matibabu ya magonjwa kama hayo pamoja na mengine ya matatizo ya kuziba kwa mishipa ya damu zinapatikana hapa nchini na hakuna haja ya kusafiri kwenda kutibiwa nje ya nchi ambako gharama ni kubwa.

Alisema matibabu ya aina hiyo nje ya nchi ni kati ya Sh. milioni 15 hadi 20 wakati hapa nchini huduma inapatikana kwa gharama nafuu.

Kwa upande wake, Fatma Khamis, ambaye alifanyiwa upasuaji huo alisema kwa muda wa miezi nane iliyopita miguu ilikuwa inamuuma baadaye akapata kidonda ambacho hakikupona hata baada ya kwenda Hospitali. Alisema baadaye alikwenda kwa daktari wa mifupa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja iliyopo Zanzibar ambapo baada ya kufanyiwa vipimo aliambiwa anatatizo la damu kuganda na kupewa rufaa ya kwenda kutibiwa katika hospitali ya JKCI iliyopo Dar es Salaam kwani hospitali hiyo haikuwa na uwezo wa kumtibu.

"Baada ya kufika JKCI nilifanyiwa vipimo na kuambiwa mshipa mkubwa wa damu haupitishi damu katika miguu na hivyo kutakiwa kufanyiwa upasuaji wa kupandikiza mishipa ya damu niliambiwa katika upasuaji huo naweza kupona au la na hivyo kupewa fomu za kusaini nikasaini," alisema.

Alisema baada ya kufanyiwa upasuaji yuko vizuri kwani anaweza kusimama na kutembea vizuri maumivu ya miguu yamepungua tofauti na alivyokuwa mwanzo.



Ofisa Mkuu Mkaguzi wa Ndani wa Benki ya NMB, Juma Kimori, akizungumza wakati wa kongamano la wafanyabiashara wakubwa lililoandaliwa na NMB jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# WB yasaidia magari 14 mradi kukuza utalii

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BENKI ya Dunia kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania kupitia mradi wa kusimamia maliasili na kukuza utalii (Re Grow), imekabidhi magari 14, yenye thamani ya Sh. Bilioni 1.5 ili kukuza sekta ya utalii katika hifadhi za kusini.

Akizungumza katika hafla fupi ya makabidhiano ya magari hayo, Kamishina Mkuu wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Dk. Allan Kijazi, alisema magari hayo yatasaidia kupambana na ujagiri na kukuza utalii katika hifadhi zilizopo ukanda wa kusini.

Dk. Kijazi, alisema kupitia mradi huo serikali imepanga kuboresha miundombinu ya hifadhi zilizopo kusini mwa nchi ili kupanua wigo kwa watalii wengi kuzitembelea.

Alisema, hivi sasa hifadhi za kanda ya kaskazini ndizo zimekuwa zikifanya vizuri kwa kutembelewa na idadi kubwa ya watalii, hivyo jitihada zinahitajika kukuza utalii katika kanda ya kusini. "Pamoja na magari haya lakini mradi huu pia utasaidia katika kuboresha hifadhi zilizopo kanda ya kusini kwa kurekebisha miundombinu kwa kufungua barabara na kujenga viwanja vya ndege kwajili ya watalii kutua na ndege katika maeneo ya hifadhi," alisema Dk. Kijazi.

Pia alisema kuwa, magari hayo yatapelekwa katika hifadhi ya Ruaha, Mikumi na Udizungwa na magari mengine tisa yatakuja hivi karibuni kwa ajili ya hifadhi mpya ya Nyerere, na kufikia idadi ya magari 23, yenye thamani ya Sh. bilioni 2.5.

"Mradi huu ni wa miaka sita utagharimu dola milioni 60, tunatoa shukrani zetu kwa Benki ya Dunia na serikali yetu ya Tanzania, kwa kusaini mkopo huu na kuthamini mchanago wa sekta ya utalii nchini," alisema Dk. Kijazi.

Mwenyekiti wa bodi ya TANAPA, Jenerali mstaafu George Waitara, alisema mradi huo utasaidia kuimarisha sekta ya utalii nchini, kwa kuboresha miundombinu mbalimbali katika hifadhi zote za kusini ili kuvutia utalii. Alisema, pia mradi huo utasaidia katika kuimarisha shughuli mbadala katika hifadhi na kuimarisha usimamzi wa mazingira.

"Mradi huu pia utasaidia kuboresha hifadhi katika nyanda za kusini mwa nchi yetu," alisema.

Kadhalika, alisema pia changamoto zilizopo hivi sasa katika hifadhi za kanda ya kusini mwa nchi ni miundombinu duni hivyo kusababisha watalii kushindwa kufika katika maeneo yote ya hifadhi.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, aliagiza magari hayo yatumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

Kanyasu alisema kuwa, zinahitajika jitihada kubwa za uwekezaji, katika hifadhi zilizopo kanda ya kusini ili kufikia kama zile za kanda ya kaskazini ambazo zinafanya vizuri hivi sasa katika sekta ya utalii nchini.

HABARI KITAIFA

# Wafanyabiashara wanawake waomba benki ziwasaidie

**Na Yasmine Protace**

WAFANYABIASHARA wanawake wa mipakani, wameziomba benki ziwasaidie kuwainua kiuchumi ili wanufaike na biashara wanazofanya.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa wafanyabiashara hao, Beatrice Yohana, katika mafunzo ya siku mbili ya kuwajengea uwezo wa kufanya biashara za na kuinuka kiuchumia kupitia taasisi za kifedha.

Aliushukuru Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kwa kutambua changamoto ambazo zinawakuta wanawake wafanyabiashara wa mipakani na kuamua kuwaandalia mafunzo ambayo yatawasaidia kujiinua kiuchumi.

"Benki zinatakiwa kutuwezesha kiuchumi wafanyabiashara wanawake wenye mitaji midogo, badala ya wenye mitaji mikubwa," alisema.

Aliongeza kuwa wanapowainua kiuchumi na inakuwa rhisi kuzitangaza benki zao.

Aliongeza kuwa changamoto nyingine ambazo wanakumbana nazo ni baadhi ya wafanyabiashara kutojua sheria pamoja na baadhi ya benki kutoa mikopo iliyo na tiba kubwa.

Faith Swai, Ofisa kutoka Benki ya Equity, ambaye alitoa mada, alisema kuwa wafanyabiashara hao wamepatiwa elimu ya fedha ikiwamo na utunzaji ili waweze kuinuka kiuchumi.

Alisema mbali na elimu ya kutunza fedha, pia wamepatiwa elimu ya kunufaika na fursa zilizopo katika mabenki.

Alisema wamekuwa wakitoa mafunzo kwa kinamama wafanyabiashara mipakani kutokana na benki yao kuwapo mipakani.

Ofisa kutoka Benki ya CRDB, alisema changamoto ambayo wanaiona katika ofisi yao ni baadhi ya wafanyabiashara kuomba mikopo muda ukiwa umekwisha hali inayosababisha kutopata mikopo.

"Tunatoa mikopo, tatizo lililopo mtu anakuja kuomba mikopo bajeti iliishapita, sasa kama bajeti imepita mtu hawezi kupata mkopo," alisema.

Aliongeza benki hiyo imekuwa ikiwawezesha wanawake ili wainuke kiuchumi.



Mkuu wa Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, Edward Mpogolo (kushoto), akizungumza na wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya hiyo, viongozi wa kata ya Mwaru na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, wakati akikagua Msitu wa Minyughe ambao umevamiwa na kufanyiwa uharibifu mkubwa wa mazingira. **PICHA: DOTTO MWAIBALE**

# Wadau waombwa mpango kudhibiti taka

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI za Mitaa nchini kwa kushirikiana na wadau wengine zimetakiwa kuweka mpango maalum wa kuelimisha jamii namna ya kudhibiti taka na kuepuka kuzitupa ovyo hali ambayo ni hatari kiafya.

Taka hizo ni pamoja na barakoa zilizokwisha kutumika, ambazo baadhi ya watu huzitupa ovyo mitaani badala ya kuziweka kwenye chombo ya kutunzia taka ili baadaye zichomwe moto.

Wito ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mtaalam Mshauri wa Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Hussein Omary, wakati akizungumza kwenye kongamano, Urafiki jijini Dar es Salaam.

Kongamano hilo lililopewa jina la Taka ni Ajira, liliandaliwa na Jukwaa la Vijana Ubungo, lenye lengo la kuhamasisha vijana kujiajiri kupitia ukusanyaji taka mitaani.

"Ni wakati mwafaka wa Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kwa kushirikiana na wadau wengine kuweka mpango maalum wa kuelimisha jamii namna ya kudhibiti taka zikiwamo barakoa zilizokwisha kutumika ili kulinda afya na mazingira," alisema Dk. Omary.

Alisema, hatua hiyo inaweza kuhusisha jamii kuziharibu barakoa baada ya kuzitumia, kwa kuweka vyombo vya kuhifadhia taka katika maduka ya dawa kama sehemu ya kuhifadhia barakoa hizo au kuwaelimisha watoa huduma ya uzoaji taka kuzitenganisha barakoa wakati wa kuzikusanya.

"Wazoa taka wanaweza kutenganisha barakoa na taka nyingine wakati wa kuzikusanya na kuzipeleka kwenye hospitali za serikali kwa ajili ya uteketezaji, hivyo ni matumaini yangu, mikakati hii na mingine ambayo inaweza kutolewa na wataalamu wa afya inaweza kupunguza kama si kuondoa hatari ya maambukizi ya magonjwa mbalimbali kwa jamii," alisema.

Dk. Omary alisema Kifungu cha 137 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kinampa mamlaka waziri mwenye dhamana ya usimamizi wa mazingira kwa kushirikiana na waziri mwenye dhamana ya usimamizi wa masuala ya afya kuhakikisha taka zinatokana na masuala yahusuyo afya ikiwamo barakoa kutenganishwa na kuhifadhiwa vizuri ili zisisababishe maambukizi ya magonjwa mbalimbali na kuha-

## Wateja Tigo kununua tiketi boti za ZanFast

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI simu za mkononi Tigo, imeingia katika makubaliano na Kampuni ya usafirishaji ya Vigor Group ambayo inamiliki boti za ZanFast Ferries ili kuwawezesha wateja wake kununua tiketi kwa njia ya Tigo Pesa.

Imeelezwa kuwa, hatua hiyo itaboresha huduma za ukataji tiketi kwa wateja wao.

Kampuni ya ZanFast Ferries ni moja ya watoa huduma za usafiri wa majini kati ya Zanzibar na Dar es Salaam zinazochangia katika urahisishaji wa huduma za usafiri kwa wenyeji na wageni.

Kaimu Mkuu wa Huduma za Kifedha wa Tigo Pesa, Angelica Pesha, alisema: "Tukiwa kama kampuni inayoongoza katika huduma za kidigitali Tanzania, tunafuraha kwa hatua hii kwani inaongeza thamani katika huduma zetu.

Kwa sasa wateja wanaweza kununua tiketi kirahisi zaidi kwa Tigo Pesa mahali popote walipo.Tunawashauri wateja wetu kutumia huduma hii ili kuokoa muda na kulipa kwa urahisi zaidi."

"Tunaamini njia hii ni suluhu ya muda mrefu na itaboresha namna wateja wanavyopata huduma za usafiri hususan wasafiri wa ndani kwani kwa sasa hakuna haja ya kwenda tena katika ofisi bali ukiwa na simu yako tu unaweza kujihakikishia uhakika wa kupata usafiri," alisema Pesha.

Mkurugenzi Mkuu wa Vigor Group, Toufiq Turky, alieleza kufarijika na ushirikiano kati yao na Tigo Pesa kwani huduma ya Tigo Pesa ni huduma ya uhakika na rahisi kutumika mahali popote na kwamba itarahisisha upatikanaji wa huduma za usafiri kwa wateja wake.

"Ushirikiano baina yetu na Tigo Pesa umetanua wigo wa njia za malipo sanjari na App yetu ya ZanFast Ferries ambazo zinampa mteja uhuru wa kununua tiketi mahali popote alipo," alisema Turky.

Aliongeza kuwa kampuni hiyo itaendelea kushirikiana na Tigo katika kuleta huduma na bidhaa za kidigitali ili kurahisisha malipo kwa wateja wake.

## Wananchi waonywa kujihusisha na rushwa uchaguzi mkuu

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WANANCHI wameonywa kuichukia rushwa kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu ili waweze kupata thamani ya kura watakazowapigia viongozi.

Wameelezwa kuwa kwa kufanya hivyo, watapata maendeleo, kuishi kwa amani, utulivu na haki katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Hayo yalisemwa na viongozi wa Taasisi ya Kuzuwia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilayani Tunduru mkoani Ruvuma Manziro Mkumba na Mkuu wa Taasisi hiyo Wilaya ya Tunduru Daudi Kambona, na kwamba taasisi hiyo imejipanga kuelimisha wananchi wa wilaya hiyo.

Walisema kuwa taasisi hiyo imeandaa utaratibu wa kutoa elimu hiyo kupitia njia mbalimbali vilabu vya wapinga rushwa mashuleni, mikutano ya hadhara na kuwafanya wananchi waichukie rushwa.

Pia wasikubali kuchagua viongozi wanaotoa rushwa kwani ikitokea wamepata madaraka hawatawahudumia badala yake watafanya kazi ya kurejesha fedha zao kwanza.

Walisema pia wanatoa nafasi kwa wananchi kutoa taarifa za vitendo vya rushwa.

Walisema pia wanawahamasisha wananchi kutoa taarifa kwa kupiga simu ya bure katika ofisi zao zilizopo Tunduru, mkoani na makao makuu.

Walisema pia taasisi imekuwa ikifanya utafiti na kubaini viashiria vya rushwa na kuielewesha jamii hasa wakati huu wa kuelekea kwenye uchaguzi mkuu kwa kufuta sheria ili kuwawezesha wananchi kuchagua viongozi.

Walisema zipo sheria zinazowaongoza katika ufuatiliaji wa vitendo ambavyo vinaweza kufanywa na wagombea vikiwamo vitendo vya kuwashawishi wananchi kwa kutoa ahadi na kutoa hongo na kuwafanya wananchi kumchagua kiongozi anayestahili kuwatumikia wengi.

Wakiongea kwa nyakati tofauti baadhi ya Wananchi pamoja na kuwapongeza maofisa hao kwa kujipanga kutoa elimu hiyo, walisema kwa sasa sehemu kubwa ya wananchi imeelimika kutokana na kudanganywa na wagombea kwenye majukwaa.

# RC Ndikilo aonya wazazi kesi za mimba

**Na Julieth Mkireri,** RUFIJI

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amesema wazazi na walezi watakaobainika kumaliza kesi za mimba nje ya mahakama watachukuliwa hatua za kisheria.

Ndikilo aliyasema hayo hivi karibuni alipokuwa katika ziara ya kikazi katika Wilaya ya Rufiji, ambapo alitembelea Shule ya Sekondari ya Mkongo na kuzungumza na baadhi ya wazazi, walimu na wanafunzi.

Ndikilo alisema suala hilo sio la kulitetea, na kwamba Serikali ya mkoa huo haitanyamaza kwa mzazi anayefanya maelewano na mtuhumiwa aliyempatia mimba mwanafunzi.

"Tulishasema anayempa mimba mwanafunzi wa kike sio suala la kumalizana kifamilia ni la mahakamani na si vinginevyo, tunataka mtoto wa kike alindiwe haki zake" alisema Ndikilo.

Alisema, Serikali wataendelea kuwa wakali kwa wazazi na walezi wa watoro na wanaofumbia macho suala la kuwachukulia hatua watuhumiwa wa kesi za mimba.

Aliwataka wanafunzi kuacha kuwa na tamaa wakiwa shuleni badala yake kuzingatia masomo kwani hakuna taifa lenye maendeleo bila ya elimu.

Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Luteni Kanali Patrick Sawala, aliahidi kufuatilia maagizo yaliyotolewa na mkuu wa mkoa katika kukomesha mimba na utoro.

Mkuu huyo wa mkoa alisema ifikapo kesho shule zote zenye upungufu wa madawati, tatizo hilo litakuwa limetatuliwa kutokana na kazi ya kutengeneza samani hizo inayoendelea.



Sehemu ya waandamanaji wa madhehebu ya Shia wakiwa katika maandamano ya amani ya kuadhimisha mwezi Mtukufu wa Muharram sambamba na kumbukumbu ya kifo cha mjukuu wa Mtume Muhammed (SAW), Imam Hussain. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yaja na mikakati kukuza utalii nchini

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imesema kuwa inathamini sana sekta ya utalii nchini na imeweka mikakati endelevu zaidi katika kuhakikisha shughuli za utalii zinakua zaidi nchini.

Kauli hiyo ilitolewa na Meneja wa matawi ya Zanzibar, Abdallah Duchi, wakati wa mkutano wa wadau wa utalii Zanzibar uliofanyika hoteli ya Verde, chini ya udhamini wa benki hiyo.

Alisema benki hiyo inajipanga vyema kutoa suluhisho la huduma za kifedha, kwa kuwa na mifumo bora zaidi wa ubadilishaji fedha na biashara ya kadi.

Alisema hatua hiyo imewezesha watalii kutohangaika wanapofanya ununuzi na malipo mbalimbali kwa kushirikiana na hoteli na baadhi ya kampuni ya utalii kwa kugawa mashine za malipo (POS) na pia kuimarisha mfumo wa malipo ya mitandano (E-Commerce). "Kwa Zanzibar na hata Tanzania Bara, utalii unachangia kwa kiasi kikubwa sana katika pato la taifa, na kwa Zanzibar zaidi ya asilimia 80 ya fedha za kigeni katika hazina ya serikali zinatokana na utalii," alisema.

Naye Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, ameitaka jumuiya ya waratibu wa misafara ya Utalii Zanzibar 'ZATO' kuendelea kuchukua jitihada za makusudi katika kuhamasisha na kuboresha utalii wa ndani na kuacha kutegemea wa nje pekee.

Akifungua mkutano wa pili wa Jukwaa la Utalii, alisema ni vyema kuhamasisha vijana wa kizanzibar kutembelea vivutio mbalimbali kwani ulimwengu umetawaliwa na mitandao na wengi wanafahamu kutumia, hivyo ni rahisi kusambaza vivutio hivyo duniani kwa muda mchache.

Pia alisema ni jukumu kutangaza haiba na upekee wa vivutio vya utalii vilivyopo na kuacha kuwategemea watu kutoka mataifa mengine kuja kutangaza vivutio hivyo ndani ya nchi.

Alisema Zanzibar inategemea sekta ya utalii kama njia kubwa ya kukuza pato la Taifa huku ikifuatiwa na biashara pamoja na shughuli za Kilimo.

Balozi alisema Mwaka 2019 utalii ulichangia shilingi bilioni 833.4 za pato la Taifa ukilingaanisha na Sh. bilioni 712.7 kwa mwaka 2018.

Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mohmoud Thabit Kombo, ameitaka Wizara ya fedha kuweka mipango kwa kuwashajihisha wafanyabiashara ili kushajihisha vivutio vya utalii.

Mwenyekiti wa ZATO, Hassan Ali Mzee, akiwasilisha mada alisema kufanyika kongamano hilo kutatoa nafasi kubwa kwa wadau na kujipanga upya kuboresha utalii.

Mkuu wa Idara ya Biashara za kadi wa NMB, Philbert Casmir, alisema wanaimarisha huduma kwa kuhakikisha watalii wanapata huduma kupitia matawi ya benki hizo hasa pale yanapotokezea majanga.

Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Abdalla Mohamed Juma, alisema mikakati ya Serikali kuendeleza utalii wa ndani na nje kwa kushirikiana na jumuiya za waratibu misafara.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 10 BORA WA UEFA MSIMU 2019-20 UK. 12&13



# CHIPUKIZI WATANO WALIOSHINDA TAJI LIGI YA MABINGWA ULAYA

**LISBON, Ureno**

BAYERN Munich ilishinda taji la Ligi ya mabingwa Ulaya kwa kuichapa Paris Saint-Germain 1-0 kwenye fainali, bao likifungwa kwa kichwa na Kingsley Coman. Bavaria hao sasa wameshinda taji hilo kwa mara ya sita.

Kuchomoza kwa wachezaji kama Alphonso Davies na Erling Haaland kulifanya mashindano hayo kuvutia zaidi. Davies alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu kwa Bayern msimu huu na mengi zaidi yanatarajiwa kutoka kwake.

Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na wachezaji ambao wameshinda taji hilo wakiwa na umri mdogo.

Makala hii inawaangalia wachezaji watano ambao walishinda taji hilo wakiwa chipukizi wenye umri mdogo.

Muhimu: Wachezaji hao ni wale tu walioanza kwenye mchezo wa fainali.

**#5 OWEN HARGREAVES, BAYERN MUNICH | Miaka 20, Miezi 4 na siku 3.**

Alizaliwa Canada, Owen Hargreaves alijiunga na akademi ya Bayern Munich mwaka 1997, akicheza mechi za kwanza kwa klabu hiyo mwaka 2000.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England alikuwa nguzo muhimu ya kiungo kwa Bavaria hao. Alianza kwenye mchezo wa fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya, ambapo Bayern Munich walishinda kwa penalti 5-4 dhidi ya Valencia.

Hargreaves aliondoka Bayern Munich kwenda kucheza kule Manchester United mwaka 2007, lakini majeruhi ya mara kwa mara yakaathiri muda wake klabuni hapo. Baada ya kwenda kucheza kwa muda kule Manchester City, Hargreaves alistaafu soka mwaka 2012 na sasa ni mchambuzi.

**#4 ALPHONSO DAVIES, BAYERN MUNICH | Miaka 19, Miezi 9 na siku 21**

Alphonso Davies ameshinda taji hilo msimu huu 2019-20 akiwa na Bayern Munich.

Nyota huyu wa kimataifa wa Canada alijiunga na Bayern Munich kutoka Vancouver Whitecaps Januari mwaka 2019. Alikuwa akicheza kama winga wa kushoto wakati wake akicheza kwenye Ligi Kuu ya Marekani, MLS, lakini Davies alianza kuichezea Bayern Munich kama mlinzi wa kushoto.

**#3 CARLOS ALBERTO, PORTO | Miaka 19, Miezi 5 na siku 15**

Alikuwa sehemu ya kikosi cha FC Porto kilichoishangaza duniani kwa kushinda taji la Ligi ya mabingwa Ulaya mwaka 2004, na Carlos Alberto alikuwa nguzo muhimu sana kwenye mchezo wa fainali dhidi ya AS Monaco.

Alberto alijiunga na Porto akitokea Fluminense Januari 2004, na haraka akawa nyota kwa kikosi cha kocha, Jose Mourinho. Mchezaji huyo wa kimatafa wa Brazil alianza kwenye mchezo wa fainali kwa Porto, na alifunga bao la ufunguzi katika ushindi wa 3-0 dhidi ya Monaco. Aliondoka klabuni hapo mwaka 2005 na kwenda kujiunga Corinthians.

Baada ya kukaa na Fluminense, Werder Bremen, Vasco da Gama na Botafogo, Alberto alistaafu soka mwaka 2019, na kwa sasa ni mchambuzi.

**#2 CLARENCE SEEDORF, AJAX | MIAKA 19, Mwezi 1 na siku 21**

Mmoja wa vungo bora wa wakati wote, Clarence Seedorf ambaye alishinda taji la Ligi ya mabingwa Ulaya mara nne na klabu tatu tofauti, akianza na Ajax.

Ni zao la academi ya Ajax, mchezaji huyu wa kimataifa wa Uholanzi alikuwa nguzo muhimu ya kiungo kwa kikosi cha Ajax kilichokuwa kinanolewa na kocha, Louis van Gaal, akitengeneza upatina mzuri na Edgar Davids na Patrick Kluivert. Alianza kwenye fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya msimu wa 1994-95 dhidi ya Milan, kabla ya kutolewa kipindi cha pili.

Aliondoka Ajax mwaka 1995 na alicheza katika timu za Real Madrid, Inter Milan na AC Milan, ambako kote alikuwa na mafanikio makubwa. Alistaafu soka mwaka 2014, baadae akawa kocha wa AC Milan, Deportivo La Coruna na Cameroon kwa nyakati tofauti.

**#1 IKER CASILLAS, REAL MADRID | MIAKA 19 na siku 4**


Ni gwiji wa Real Madrid, Iker Casillas anatajwa kama mmoja wa magolikipa bora zaidi wa wakati wote.

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Hispania ni zao la akademi ya Real Madrid, na alianza kuichezea klabu hiyo mwaka 1999. Amecheza hapo Real Madrid kwa miaka 16.

Aliondoka klabuni hapo mwaka 2015 kwenda Porto, ambako alikaa miaka minne kama golikipa namba moja. Alistaafu mwaka 2020, na kwa sasa ni mshauri wa rais wa Real Madrid, Florentino Perez.

## ISIKUPITE

Fowadi wa Barcelona, Antoine Griezmann, alitaka kuondoka pale Camp Nou kabla ya kuzungumza na kocha mpya, Ronald Koeman, ambaye alimhakikishia kuwa yupo kwenye mipango yake.





# WACHEZAJI 10 BORA WA UEFA MSIMU 2019-20

**LISBON, Ureno**

MSIMU wa 2019-20 hatimaye ulimalizika kwa fainali ya ligi ya mabingwa Ulaya. Bayern Munich iliifunga Paris Saint-Germain bao 1-0, likifungwa kwa kichwa na Kingsley Coman na wakalibeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya sita katika historia yao.

Kuna vingi vya kukumbukwa vilivyotokea kwa msimu mzima; ikiwamo kuchomoza kwa Erling Haaland, mabao manne ya Serge Gnabry dhidi ya Tottenham Hotspur, na kichapo cha historia walichokumbana nacho Barcelona wakati wakitandikwa 8-2 na Bayern Munich kwenye robo fainali.

PSG hii ilikuwa fainali yao ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kikosi hicho cha kocha, Thomas Tuchel kuwafunga Atalanta na RB Leipzig kuelekea wenye fainali hiyo. Hata hivyo, kikosi cha kocha Hansi Flick, Bayern Munich kilikuwa bora zaidi, na kilistahili kubeba taji.

Bavaria hao walimaliza msimu kwa kushinda mataji matatu, na kuifikia rekodi ya Barcelona kuwa timu pekee kumaliza msimu kwa kubeba mataji matatu mara mbili mfululizo.

Hapa tunawaangalia wachezaji 10 bora wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

#10 DAVID ALABA - BAYERN MUNICH

Mmoja wa wachezaji wa kazi wa Bayern Munich kwa sasa, David Alaba, kiukweli kabisa ameitendea haki nafasi yake ya ulinzi kwa Bavaria msimu huu.

Ana uwezo wa kucheza kama mlinzi wa kushoto, mlinzi wa kati, kiungo au winga, nyota huyu wa kimataifa wa Austria amekuwa na ubora wa kuvutia zaidi hasa kwa kutengeneza upatina wake na Jerome Boateng.

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 28 pengine mchezo ule wa fainali unaweza kuwa ulikuwa wa mwisho kwake kuwachezea Bayern. Huku mkataba wake ukiwa umebakiwa na mwaka mmoja, Alaba amekuwa akihusishwa na baadhi ya klabu kubwa duniani, ikiwamo Barcelona, Real Madrid, Juventus na Manchester City.

#9 ERLING HAALAND - RED BULL SALZBURG/BORUSSIA DORTMUND

Anatajwa kama mshindi ajae wa tuzo ya Ballon d'Or, Erling Braut Haaland amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wachezaji bora vijana duniani.

Mchezaji huyo wa kimatafa wa Norway awali alitamba kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi akiwa na Red Bull Salzburg; akawa mchezaji wa kwanza kufunga mabao sita katika mechi zake tatu za mwanzo kwenye michuano hiyo. kwa ujumla katika mechi sita alizoichezea Salzburg kwenye mashindano haya, amefunga mabao nane.

Uhamisho wa euro milioni 20 kwenda Borussia Dortmund ulifanyika Januari, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 alifunga mabao mawili dhidi ya Paris Saint-Germain kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16. Haaland alifunga mabao 10 katika mechi nane tu za mashindano hayo, akimaliza nafasi ya pili nyuma ya Robert Lewandowski kwa ufungaji bora.

#8 KEVIN DE BRUYNE - MANCHESTER CITY

Ndiye mchezaji bora wa Ligi Ku ya England msimu huu, Kevin De Bruyne pia alikuwa na mchango mkubwa kwa Manchester City kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya.

De Bruyne alifurahia wakati wake katika mashindano hayo, licha ya Manchester City kutolewa na Lyon hatua ya robo fainali. Nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji ambaye pasi zake zina macho, alikuwa nguzo muhimu zaidi kwenye kutengeneza mashambulizi kwa kikosi chake.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 alishindwa kubadilisha mambo dhidi ya Lyon. Katika mechi saba za Ligi ya mabingwa Ulaya, amefunga mabao mawili na pasi za mwisho mbili.

#7 HOUSSEM AOUAR - LYON

Akademi ya kukuza wachezaji ya Lyon imewatoa nyota kama Corentin Tolisso, Alexandre Lacazette na Samuel Umtiti, na Houssem Aouar ndio nyota wao wa sasa ambaye ni zao la akademi hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alikuwa mmoja wachezaji bora waliofika kwenye nusu fainali ya ligi ya mabingwa Ulaya, kwa kuichapa Manchester City. Ubunifu wa Aouar ulikuwa siraha muhimu ya Lyon. Akicheza vizuri zaidi katika nafasi ya kiungo pamoja na winga ya kushoto.

Nyota huyu wa timu ya taifa ya Ufaransa chini ya umri wa miaka 21 amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka hapo Lyon, huku Manchester City, Arsenal na Juventus zikihusishwa.

#6 ANGEL DI MARIA - PARIS SAINT-GERMAIN

Wengi wanamkumbuka Angel Di Maria mara kwa mara kwa kindi chake kigumu wakati akicheza pale Manchester United, ambapo alikaa kwa msimu mmoja tu.

Wengine wanajifanya kusahau kwamba alikuwa nguzo ya Real Madrid kwenye ushindi wa kombe la Ligi ya mabingwa Ulaya wakati akicheza kule, na kiwango chake pale Paris Saint-Germain kwenye mashindano haya msimu huu ubora wake umeonekana. Akiwa amejiunga na PSG kutoka United kwa pauni milioni 44 mwaka 2015, nyota huyo wa kimataifa wa Argentina amekuwa nguzo muhimu.

Akiwa na umri wa miaka 31 amecheza mechi tisa za Ligi ya mabingwa Ulaya, akifunga mabao matatu na kutoa pasi za mwisho sita. Alikuwa patina mzuri wa Neymar na Kylian Mbappe.

#5 KYLIAN MBAPPE - PARIS SAINT-GERMAIN

Mmoja wa wachezaji bora duniani kwa sasa, Kylian Mbappe amechomoza katikati ya msimu wa wachezaji wengi bora.

Mchezaji namba mbili ghali zaidi duniani, na Mbappe amejiimarisha yeye mweyewe kwa Parisiens hao tangu alipojiunga nao mwaka 2017. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 21 alikuwa na kiwango cha kuvutia zaidi kwenye michuano hiyo wakati PSG ikitinga fainali.

Nyota huyu wa kimataifa wa Ufaransa amecheza mechi 10 katika mashindano hayo na kufunga mabao matano na kutoa pasi za mwisho tano. Kati ya mechi hizo 10, sita alianza.

#4 SERGE GNABRY - BAYERN MUNICH

Arsenal lazima watakuwa wanajutia siku waliyoamua kumuuza Serge Gnabry kwenda Werder Bremen mwaka 2016 kwa pauni milioni tano.

Msimu mmoja baadae, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani akajiunga na Bayern Munich ambapo amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi na kuwa mmoja wa mawinga bora duniani kwa sasa. Gnabry alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi kwa Bavaria kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 amecheza mechi 10 katika mashindano hayo, akifunga mabao tisa na kutoa pasi za mwisho mbili. Yakiwamo mabao manne aliyofunga dhidi ya Tottenham Hotspur wakati Bayern ikishinda 7-2 kwenye hatua ya makundi.

#3 THOMAS MULLER - BAYERN MUNICH

Ni mchezaji ambaye ni kama hayupo dimbani, lakini shughuli yake ni pevu.

Thomas Muller hachezi sana soka la kuvutia. Lakini wachache wanaofikia ubora wake. Nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani alikuwa mbunifu wa mabao na pia mfungaji.

Akiwa na umri wa miaka 30 alicheza mechi 10 kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya, saba kati yake akianza. Alifunga mabao manne na kutoa pasi za mwisho mbili.

#2 NEYMAR - PARIS SAINT-GERMAIN

Presha ya Neymar mara zote ilikuwa kubwa hadi mwisho wa mashindano hayo.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 alikuwa kwenye hatua ya makundi kwa mara ya kwanza katika mashindano hayo tangu alipojiunga na PSG mwaka 2017, na alitengeneza tofauti. Dhidi ya Atalanta alitoa mchango mkubwa zaidi, ingawa hakufunga. Dhidi ya RB Leipzig ndiye aliyeibeba timu.

#1 ROBERT LEWANDOWSKI - BAYERN MUNICH

Bilashaka ndiye mchezaji bora duniani kwa sasa, Robert Lewandowski alikuwa kwenye nafasi kubwa ya kushinda Ballon d'Or mwaka huu, kama isingefutwa.


Lewandowski amekuwa mmoja wa mastraika bora kabisa duniani kwa sasa, na alikuwa na msimu mwingine wa kuvutia zaidi. Mchezaji huyu wa kimataifa wa Poland ndiye alikuwa stelingi wa Bayern Munich. Akiwa na umri wa miaka 32 amecheza mechi 10, akifunga mabao 15 na kutoa pasi za mwisho tano. Amefunga katika mechi tisa mfululizo za Ligi ya Mabingwa, akishindwa kufunga kwenye fainali pekee.

## Nukuu

"Nani asiyemtaka Messi kwenye timu yake? Miaka sio tatizo kwetu, lakini kwakweli ni mchezaji mzuri." **Kocha wa Klabu ya Liverpool, Jurgen Klopp akizungumzia tetesi za Lionel Messi kujiunga na timu hiyo.**



"Malengo yangu ni kuwa bora zaidi nchini Italia, Ulaya na duniani nikiwa na Juventus msimu wa 2020-21," **aliandika Cristiano Ronaldo kwenye ukurasa wake Instagram akizungumzia maandalizi ya kuelea msimu mpya wa tatu akiwa na Juventus.**



"Nafikiri anatakiwa kuwa na furaha kubwa kama akiweza kubakia katika klabu hii kwa muda mrefu. Nafikiri watu watafurahia habari hizi," **alisema Mikel Arteta akiwaambia waandishi wa habari kuhusu kukaribia kusaini mkataba mpya kwa nahodha wake, Pierre-Emerick Aubameyang**



# SAJILI 10 ZILIZOBAKI KUWA TETESI

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI wa usajili duniani kunakuwa na tetesi mbalimbali za wachezaji kutoka sehemu moja kwenda nyingine na klabu moja kuhusishwa kutaka saini ya mchezaji wa klabu nyingine.

Mfano hivi sasa kuna sakata la mchezaji Lionel Messi wa klabu ya Barcelona kuwa anawindwa na klabu mbalimbali kubwa barani Ulaya.

Nchini Tanzania, tangu wakati Ligi Kuu Tanzania Bara iliposimama wakati ya ugonjwa wa COVID-19, kulikuwa na tetesi nyingi za usajili.

Pamoja na yote, tetesi wakati mwingine zinakuja kuwa kweli inatokea kama ilivyosema na wakati mwingine tetesi zinabaki kuwa tetesi. Ni kwamba hazitokei kwa sababu hakukuwa na kitu kama hicho, au dili lilikuwepo lakini halikukamilika, hivyo yote yanabaki kuwa tetesi.

Mfano mwingine ni sakata la Benalrd Morrison kusajiliwa na Simba lilianza kama tetesi hivi, wiki chache tu baada ya Yanga kuifunga Simba bao 1-0 lililofungwa na mchezaji huyo. Kila kukicha tetesi hizo zilikuwa zikienea kama moto nyikani na hivi leo imekuwa kweli, Simba imemsajili mchezaji hiyo, japo ilibidi kwanza Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji kutoa uamuzi wa kumpa ushindi kwenye kesi yake na kuwa huru.

Hata hivyo, kwenye makala haya tumekusanya taarifa zote za tetesi ambazo zilisikika sana, lakini hazikuwa kweli, au hazikukamilika wakati leo ikiwa ni siku ya mwisho ya usajili.

**1. Simba kumsajili Shonga**

Hii ilianza msimu uliopita. Simba ilihusishwa kumsajili straika huyo msumbufu kutoka Orlando Pirates ya Afrika Kusini, lakini tetesi hizo hazikuwa kweli.

Kipindi cha dirisha dogo pia kulikuwa na tetesi kama hizo, lakini pia hazikukamilika.

Msimu huu wa usajili, pia mchezaji huyo raia wa Zambia, aliandikwa sana na baadhi ya vyombo vya habari, pamoja na mitandao ya kijamii kuwa atasajiliwa, lakini tetesi zikaishia hewani.

**2. Yanga kumsajili Chama**

Kipindi cha dirisha dogo, Yanga ilitangaza kutaka kumsajili kiungo wa Simba, Cleotus Chama kitu ambacho kilimtia matatani Makamu Mwenyekiti wao Fredrick Makalebela akaomba radhi kwa sababu bado alikuwa na mkataba na Simba.

Usajili wa msimu huu, kulikuwa na tetesi za Yanga kumtaka kumsajili mchezaji huyo raia wa Zambia, na hasa tetesi zilisemwa kuwa ni kama kisasi cha kuchukuliwa mchezaji wao Morrison. Kitendo cha Chama kutua siku chache kabla ya Simba Day na kujiunga kambini, kulizima tetesi hizo.



Straika hatari wa zamani wa Nkana FC, Walter Bwalya ambaye alihusishwa kujiunga na Simba, lakini zikabaki kuwa tetesi tu. Kwa sasa anaichezea El-Gouna FC ya nchini Misri.

**3. Azam kumsajili Shiboub**

Zilipozuka tu tetesi kuwa Simba inatarajia kuachana na kiungo wao raia wa Sudan, Sharaf Eldin Shiboub, zikaanza pia tetesi za mchezaji huyo kutakiwa Azam FC. Kuna tetesi pia zilisema anapekekwa kwa mkopo. Ukweli ni kwamba mchezaji huyo alikuwa amemaliza mkataba wa mwaka mmoja na Simba, hivyo kama angesajiliwa na Azam ingekuwa ni mchezaji huru. Hadi Azam FC wanatambulisha kikosi chao, Shiboub hakuwepo, hivyo zilibaki kuwa na tetesi zisizokuwa kweli au kukamilika.

**4. Simba kumsajili Walter Bwalya**

Simba imemsajili Larry Bwalya. Huyu ni mgeni kidogo kwenye masikio wa mashabiki wengi wa soka Bongo. Lakini Bwalya si jina geni kwao. Wanaomfahamu ni Walter Bwalya ambaye kwa misimu miwili sasa amekuwa akihusishwa kutua Msimbazi, ingawa wote wawili ni Wazambia. Ni straika aliyekuwa aliicheza Nkana FC.

Kwa sasa ni mchezaji wa klabu ya El-Gouna FC ya nchini Misri. Usajili wake Simba hata msimu huu ukabaki kuwa tetesi zisizokamilika.

**5. Azam kumsajili Tshishimbi**

Baada ya kushindwana na Yanga, kiungo Papy Tshishimbi ilitajwa kuwa angetua Azam FC.

Kila mtu alisubiria muda ufike, wasikie akitajwa au kutambulishwa rasmi. Hadi klabu hiyo inatambulisha wachezaji wake, hakuwamo kiungo hiyo kutoka Congo DR na kubaki kuwa tetesi tu.

**6.Yanga kumsajili Tuyisenge**

Hata siku nne hazijapita tangu tetesi hizi zizuke. Ilisemekana kuwa Yanga ina mpango wa kutaka kumsajili straika huyu wa zamani wa Gor Mahia, raia wa Rwanda ambaye kwa sasa anaichezea Petro de Luanda ya Angola. Hata hivyo, baadhi ya viongozi wa Yanga wamekanusha taarifa hizo za kumsajili Jacques Tuyisenge.

**7. Simba kumsajili Tshishimbi**

Ni tetesi zilizokuwepo tangu dirisha dogo la usajili. Ni baada ya mchezaji huyo kusifia wachezaji wa Simba. Hata ligi ilipomalizika na kubainika hana mkataba na Yanga, ilitajwa kuwa angesajiliwa na Simba, kabla ya tetesi kugeuka na kuwa anatakiwa na Azam FC. Hakuna timu yoyote kati ya hizo mbili zilizomsajili.

**8. Yanga kumsajili Kanda**

Siku chache baada ya Simba kumsainisha Morrison, kulizuka tetesi za Yanga kutaka kulipa kisasi.

Na ilitajwa kuwa ilikuwa kwenye hatua za mwisho kumsajili Deo Kanda raia wa Congo DR.

Siku zilipita na hatimaye taarifa zinasema mchezaji huyo amejiunga na AS Vita ya nchini kwao.

**9. Azam kumsajili Kakolanya**

Ukiangalia kwenye orodha hii utagundua kuwa Beno Kakolanya ndiye Mtanzania pekee kuwemo kwenye tetesi hizi.

Golikipa huyu wa Simba ilitajwa kuwa anatakiwa na Azam FC, huku Simba ikihusishwa kusajili kipa mwingine. Hata hivyo kwenye Simba Day ametambulishwa kuwa bado yupo Simba.

**10 Simba kumsajili Nahimana**

Ni tetesi za siku nyingi kabla hata ligi ya msimu wa 2019/20 haijaisha. Ni kwamba yeye mwenyewe aliitamani klabu hiyo akiwa KMC. Raia huyo wa Burundi ambaye ni golikipa amaeikosa nafasi hiyo kwani makipa wa Simba ni walewale wa msimu uliopita. Hata hivyo habari zinasema anakamilisha taratibu za kujinga na Namungo FC.

**JE, WAJUA?**



Mshindi wa kombe la FA amemfunga bingwa wa Ligi Kuu ya England mara tano katika mechi sita za Ngao ya Jamii, huku Arsenal ikishinda mara nne katia ya hizo (2014, 2015, 2017 na 2020).



# Wanafunzi wenye ulemavu kutambuliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema inatarajia kufanya utambuzi wa wanafunzi wenye ulemavu nchini Septemba mwaka huu, ili kuweka mikakati ya kuwasaidia.

Mkurugenzi wa Elimu Maalum kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Geni Migeha, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki katika kikao cha kuwasilisha taarifa ya Mradi wa Elimu Jumuishi kwa watoto hao uliofanywa na Shirika la Sense International Tanzania kwenye Mkoa wa Dar es salaam na Kilimanjaro.

Mradi huo umefanyika kuanzia Juni 2016 hadi Mei 2020 kwa ufadhili wa Mfuko wa ubunifu kwa maendeleo ya watu (HDIF), ulioanzishwa na Serikali ya Uingereza kupitia Shirika la Misaada la Uingereza(UKAID).

Alisema mwaka juzi kwa mara ya kwanza serikali iliamua kujiridhisha kujua kuna watoto wenye ulemavu mbalimbali wangapi nchini na kubaini kuna wanafunzi wengi wenye uhitaji maalum. "Tunahitaji katika hili kusaidiwa na wadau mbalimbali ikiwamo Sense, tunalenga kuwasaidia hawa watoto na mkate umekuwa ni mdogo, tunataka tutakapowatambua wasaidiwe vifaa," alisema.

Alieleza kuwa kutokana na serikali kutekeleza mpango wa elimu jumuishi ni muhimu wakatambuliwa watoto hao na kusaidiwa.

"Mwaka juizi tuligundua tuna wanafunzi wengi wenye uhitaji maalum ikiwemo uziwi kutokuona, wapo wengi na tukaweka mikakati ya namna ya kuwasaidia," alisema.

Hata hivyo, alisema baada ya kuwatambua wanatarajia kuweka mikakati ya kuwaweka watoto hao pamoja na kuishi kwenye bweni ambapo kila mkoa uwe na shule moja.

"Bado halijaiva ni mipango yetu katika kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema wakati mwingine serikali mkono umekuwa ni mfupi kufika mahali fulani na mipango mingine imekuwa ikishindwa kukamilika lakini wataendelea kushirikiana na wadau ili kufanikisha hilo.

"Namna ya kuwasaidia watoto wenye uziwi kutokuona, mtoto anatakiwa kuwa na mwalimu anayemfundisha na msaidizi, na mtu anayemfundisha kiziwi inatakiwa iwe uwiano wa mmoja kwa mmoja, lakini hatujafikia huko bado," alisema.

Aliongeza: "Mwalimu anapomfundisha nani anamsaidia kuelewa kinachofundishwa, Sense wenzetu mmekuja na kitu mwalimu msaidizi, tutazungumza na watu wa idara ya utumishi ili kufikia mahali fulani watambulike, Sense mmeanzisha kitu ambacho serikali inafikiria kukitekeleza."

Naye, Mkurugenzi Mkazi wa Sense International Tanzania, Naomi Lugoe, alisema kwa kipindi hicho shirika hilo limefanikiwa kuwaingiza darasani watoto 100 wenye ulemavu mchanganyiko ikiwamo viziwi wasioona.

Aidha, alisema kwa mwaka huu wamepanua shughuli zao na wanatarajia kufikia shule 10 maalum ambazo zilikuwa na vitengo vya kuhudumia watoto hao. "Tunategemea kuangalia mahitaji ni yapi kwenye vituo hivyo ili kusaidia, ili kuhakikisha watoto wanakwenda shule, tupo tayari kushirikiana na serikali kuhakikisha mtoto mwenye ulemavu huo anajifunza na kufurahia maisha kama wengine," alisema.



Kijana ambaye jina lake halikufahamika, akisaga kahawa kwa kutumia mashine ndogo tofauti na wengine ambao walikuwa wakitumia kinu kutwanga zao hilo kabla ya kuwatengenezea wateja wao kinywaji cha kahawa **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Polisi yawafunda viongozi wa dini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

VIONGOZI wa dini nchini wametakiwa kuwahimiza waumini wao kutovunja amani iliyopo wakati wa uchaguzi mkuu Oktoba mwaka huu.

Kamanda wa Polisi mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alitoa wito huo jana katika semina elekezi kwa viongozi wa dini inayofanyika jijini hapa.

Muroto alisema viongozi wa dini wanapaswa kumsaidia Rais kuhimiza utunzaji wa amani ili Tanzania iendelee kuwa mfano.

"Sioni sababu ya kuvunja amani, sisi sote ni Watanzania na tunamuomba Mungu mmoja, hivyo katika uchaguzi huu tusaidie kusisitiza amani," alisema Kamanda Muroto.

Aidha, alisema Jeshi la Polisi litahakikisha harakati za uchaguzi zitakwenda sawa na kutaka kila Mtanzania awe mlinzi kwa mwenzie hususani katika kipindi cha uchaguzi mkuu.

Alisema lengo lao ni kuona Tanzania na Dodoma inakuwa na amani katika uchaguzi mkuu ambao tayari kampeni zake zimeanza.

Naye, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk.Binilith Mahenge, aliishauri jamii kutotumia mitandao ya kijamii kuvunja amani.

Dk. Mahenge alisema mitandao ya kijamii mingi, na kuwa imekuwa ikitumiwa vibaya na baadhi ya watu na kutaka mitandao hiyo itumike kuleta maendeleo na si vurugu.

Aliwapongeza viongozi wa dini walioandaa semina hiyo na itasaidia kuifundisha jamii jinsi ya kuilinda amani ya nchi.

# Tozo kero kwa wafanyabiashara kufutwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imeahidi kufuatilia na kuzifuta tozo mbalimbali ambazo zinatajwa na wafanyabiashara nchini kuwa ni kero ili kuwapa nafasi ya kufanya biashara kwa uhuru na kuchangia katika uchumi wa nchi.

Ahadi hiyo ilitolewa na Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda, Profesa Riziki Shemdoe, wakati wa kongamano la wafanyabiashara wanaowezeshwa mikopo na benki ya NMB (NMB Business Club) ambalo lilifanyika katika ukumbi wa hoteli ya Dear Mama na baadae ikafuatiwa na tafrija ya usiku katika hoteli ya Dodoma.

Profesa Shemdoe alisema Serikali itajadiliana na benki mbalimbali ikiwamo NMB ili waweke mipango itakayowezesha kila anayefanya biashara kuwa katika mazingira rafiki lakini akasisitiza suala la kulipa kodi ili kuinua uchumi wa taifa.

"Serikali itaendelea kulitazama na eneo hilo ikiwemo tozo ambazo ni kero kwa wafanyabiashara wetu kwani zinawaumiza na kuwavurugia mipango yao, lazima tuyatazame hayo na kuyaondoa, lakini NMB na benki nyingine mtazame kwa upande wenu kuhusu riba za mikopo nazo bado ziko juu," alisema Shemdoe.

Akizungumza kwenye tafrija ya usiku, Mkuu wa idara ya biashara wa NMB Alex Mgeni, alisema benki hiyo imefanya maboresho katika utoaji mikopo ambapo sasa wameanza kutoa katika kundi la wachimbaji wadogo ambao awali hawakuwemo. Mgeni alizungumzia malalamiko ya baadhi ya wafanyabiashara kuhusu tozo nyingi akawataka kuzijua sheria za kodi kwani itawasaidia kutambua kuhusu kipi wanapaswa kulipa na kwa kiasi gani.

Aliwataka wafanyabiashara kujitokeza kununua hisa za benki ili wawe sehemu ya wamiliki na kuwa fedha yao itakuwa salama zaidi kwa kuwa benki hiyo inakuwa na kwa miaka 8 imekuwa ikipata tuzo ya watoa huduma bora.

Awali Mwenyekiti wa NMB Business Club Mkoa wa Dodoma, Joyce Kaishozi, alieleza changamoto zinazowapata wafanyabiashara kutokana na ugonjwa wa Covid -19 akaomba uongozi kuwatazama kundi la wafanyabiashara.

Kaishozi alisema biashara ziliyumba katika kipindi cha ugonjwa wa virusi corona, hivyo watumishi wa benki hiyo wanapaswa kuzungumza na wateja wao kujua namna wanavyoweza kutatua changamoto zao ili waendelee na viwango vya mikopo yao.

Meneja wa NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, alisema benki hiyo imekuwa na mtandao mkubwa ikifikisha matawi 230 kwa nchi nzima, wakala 7000 na ATM wamefikisha 800 wakati kanda ya kati kuna matawi 25.

Mlozi alisema katika kanda yake yenye mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara ni Wilaya ya Chemba pekee ambayo haina tawi. Lakini aliongeza baadhi ya maeneo wanatumia matawi yanayotembea lengo ni kuwafikia wateja popote walipo.

"Mpango wa benki ni kuhakikisha inawafikia watu wote na kuwahudumia kwa kuwa wanalenga zaidi kumwondolea Mtanzania kero ya kufuata huduma maeneo ya mbali na wanapoishi," alisema Mlozi.





# Chalamila awaonya wanafunzi wa haribifu wa miundombinu

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewataka wanafunzi wa shule za msingi na sekondari mkoani humo kuepuka kufanya vitendo vya kuharibu wa miundombinu ya shule zao ili kuepuka kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Chalamila alitoa onyo hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa kwenye ziara ya kukagua miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, mabweni na maabara katika shule mbalimbali wilayani Mbarali, miradi ambayo inatekelezwa kwa ushirikiano wa wananchi na Serikali.

Alisema Serikali inatumia fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo, na kwamba kitendo cha wanafunzi kuiharibu kinasababisha hasara kubwa.

Alisema hivi karibuni aliwashughulikia wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Kiwanja wilayani Chunya waliochoma mabweni kwa kuwacharaza bakora na kuwaamuru walipe faini ambapo zaidi ya sh. Milioni 100 zilipatikana na zikatumika kujenga mabweni mapya.

"Sasa hivi ikitokea wanafunzi wengine wakafanya tukio kama hilo, hatutawachapa wala kuwatoza faini na badala yake tutawapeleka kusikojulikana na watarudi kujenga majengo hayo wakiwa wamevalia sare za magereza kwa hiyo msijiingize huko," alisema Chalamila.

Vilevile, alisema katika shule ya Sekondari ya kutwa ya Mbeya (Mbeya Day) kumeripotiwa baadhi ya wanafunzi kuwa na tabia mbaya kiasi kwamba wanafikia hatua ya kuwakunja walimu wao wakitaka kupigana nao.

Alisema vitendo hivyo ni utovu wa nidhamu na vinawafanya wanafunzi kutofanya vizuri kwenye masomo, hivyo aliwataka wanafunzi hao kuacha tabia hiyo kwa maelezo kuwa vitawagharimu.

Awali akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema inatekelezwa kwa ushirikiano kati ya wananchi na Serikali kuu ambapo alisema Serikali imetoa fedha kwa njia tofauti tofauti.

Alisema baadhi ya miradi hiyo inatekelezwa kupitia mfumo wa lipa kulingana na matokeo (EP4R) na kwamba miradi inayotekelezwa kwa mfumo huo ni ujenzi wa bweni la wasichana, matundu ya vyoo na vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Mengele.

Alisema lengo miradi mingine ya ujenzi wa miundombinu hiyo inatekelezwa katika shule za Sekondari Iwindi na Mwakaganga pamoja na Shule ya Msingi Isisi ambako vinajengwa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo.

"Wananchi wanachangia nguvu zao kwa kuleta mchanga, mawe na tofali lakini Serikali imetoa fedha ambazo zinatumika kununua vifaa vingine na vilevile wananchi wanashiriki kwenye ujenzi," alisema Mfune.

Baadhi ya wanafunzi waliishukuru Serikali kwa kuwaboreshea miundombinu huku wakiiomba kuboreshewa mazingira mengine yaliyobakia ikiwamo upatikanaji wa vitabu vya kiada na ziada.

Mmoja wa wanafunzi hao, Zacharia Abdalah, ambaye ni mwanafunzi wa Kidato cha tano katika Shule ya Sekondari Mengene, alisema maktaba ya shule hiyo haina vitabu vya kutosha na hivyo wanashindwa kujisomea.

Vilevile, alisema shule hiyo haina Mwalimu wa Somo la Hisabati na hivyo wanalazimika kumtumia mwalimu anayetoka katika Shule ya Sekondari Rujewa ambaye anaenda mara moja moja shuleni hapo.

# Machifu wakiri mfumo dume katika jamii

**Na Grace Mwakalinga**
MBEYA

JUMUIYA ya Machifu mkoani Mbeya imekiri kuwa baadhi ya familia bado zinaendekeza mfumo dume dhidi ya wanawake hali inayosababisha kundi hilo kukosa haki zao za msingi kama vile elimu, umiliki wa mali na uongozi.

Pia wamesema bado wanawake na watoto katika jamii wanakosa haki zao za msingi ikiwamo umiliki wa mali, haki ya kupata elimu na fursa za mbalimbali za uongozi kwa sababu ya kuendekeza mfumo dume.

Hayo yalisemwa jana na Chifu wa Kabila la Wasafwa mkoani Mbeya, Roketi Mwashinga, wakati wa mkutano wa kujadili mtazamo wa dini ya kiafrika na madhehebu ya kikristo juu ya imani jumuishi na usawa wa kijinsia.

Alisema jamii bado inaamini mwanamke hastahili kupata haki sawa na mwanamume, hivyo anatengwa katika baadhi ya mambo hasa yahusuyo umiliki wa mali, uongozi na baadhi ya vyakula.

Alidai kupitia mjadala huo ambao uliwakutanisha pamoja viongozi wa dini kutoka madhehebu mbalimbali ya ndani na nje ya Mkoa wa Mbeya kujadili nini kifanyike katika kuweka usawa wa kijinsia, ni vyema sasa Serikali ikasimamie sera na mikataba ya kimataifa ambayo inamlinda na kumpa haki mwanamke.

"Sisi machifu tunakiri kuwa bado kuna mfumo dume katika jamii yetu, tumeshuhudia na wakati mwingine tunaamua kuingilia kati ukatili wa kijinsia, moja ya sababu ya hali hiyo ni wazazi kuwagawa watoto kati ya msichana na mvulana kuanzia majukumu na huduma... utashangaa mtoto wa kike anaambiwa huwezi kusimama katikati ya wanaume au huwezi kula firigisi au maini ni ya mtoto wa kiume, jambo ambalo halina mashiko," alisema Mwashinga. Aliongeza kuwa katika kutekeleza masuala ya jinsia katika kabila la Kisafwa waliamua kumpa uchifu mwanamke mmoja kutoka Mji wa Mbalizi, na kwamba anaongoza vizuri eneo lake kwa hekima na busara kuliko ilivyodhaniwa kubwa huenda hataweza.

Chifu msaidizi wa kabila hilo, George Lyoto, alisema vitendo vya ukatili wa kijinsia vimewafanya wanawake wakose ujasiri wa kujiamini na kujiona dhaifu.

Alisema moja ya njia ya kukomesha vitendo hivyo ni viongozi wa dini, machifu, serikali na wadau wengine kushirikiana kwa pamoja katika kutoa elimu kwa wananchi kuripoti matukio ya ukatili yanapotokea.

Mchungaji Marry Kategile, Mkurugenzi wa Elimu Anuai kutoka katika Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji, alisema viongozi wa dini wana nafasi kubwa ya kutokomeza masuala ya ukatili na kuhimiza usawa wa kijinsia kupitia mahubiri yao, lakini pia katika masuala ya kiutendaji.

Alisema dhana ya usawa wa kijinsia vile vile inahusisha mgawanyo sawa wa uongozi katika makanisa kwa kuhakikisha kuna asilimia ya uongozi kati ya mwanaMume na mwanamke.

Naye Naibu Makamu Mkuu wa Chuo hicho (Taaluma), Profesa Tully Kassimoto, alisema kuwa suala la uongozi kwa wanawake liko nyuma kwa madai kuwa mwaka 2015 ni asilimia sita tu ya wabunge wanawake.

Katibu Mkuu wa Kanisa la Moravian nchini, Mchungaji David Mgombele, alisema kuwa mila na desturi zinachangia kumkandamiza mwanamke kuanzia ngazi ya familia ambapo mtoto wa kiume anapewa kipaumbele katika kusoma na masuala mengine muhimu ukilinganisha na mtoto wa kike.



Chifu wa kabila la Wasafwa mkoani Mbeya, Roketi Mwashinga, akitoa msimamo wao juu ya kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kinjinsia na kuhimiza usawa kati ya mwanamke na mwanamume mwishoni mwa wiki. **PICHA NA GRACE MWAKALINGA**

# Mil. 200/- kujenga madarasa DIT Songwe

**Na Grace Mwakalinga,**
MOMBA

SERIKALI imeahidi kutoa Sh. milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa matano katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Kampasi ya Myunga iliyopo wilayani Momba katika Mkoa wa Songwe.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa bwalo la chakula lililojengwa kwa fedha zilizotolewa na serikali kupitia wizara hiyo.

Alidai ombi la kutoa fedha kiasi cha Sh. milioni 200 lilitolewa na wanafunzi wa chuo hicho kuomba serikali kuboresha miundombinu ya kujifunzia pamoja na madarasa, uwanja wa michezo na vifaa vya michezo pamoja na gari la kwa ajili ya kwenda kwenye mafunzo viwandani.

Dk. Akwilapo alisema anaamini kwa fedha hizo, DIT itajenga madarasa mazuri yenye ubora unaofaa kwa kutumia wataalamu wa ndani wa Taasisi hiyo.

"Ninaipongeza DIT kwa usimamizi mzuri wa rasilimali fedha uliofanikisha kukamilika ujenzi wa chuo hicho kampasi ya Myunga mkoani Songwe kwa asilimia 100 na katika kuboresha zaidi tumeongeza fedha nyingine Sh. milioni 200 ili kukamilisha kabisa miundombinu chuoni hapo, lengo letu ni kuona wanafunzi wanapata elimu katika mazingira rafiki na yenye utulivu," alisema Dk. Akwilapo.

Kwa upande wake Mkuu wa DIT Dar es Salaam, Profesa Preksedis Ndomba, alishukuru serikali na Katibu Mkuu kwa kuendelea kuwapatia fedha za kujenga na kukarabati miundombinu ya majengo kupitia wizara hiyo na kuahidi kuendelea kusimamia vyema miradi inayowekezwa na serikali katika Taasisi.

Nae Mkurugenzi wa Kampasi ya DIT Myunga, Dk. Frank Lujaji, alisema licha ya Serikali kupitia Wizara ya Elimu kutoa kiasi hicho cha fedha, lakini pia imemlipia ada ya masomo mwanafunzi wa Tehama, Nozen Mkubwa ambaye alishindwa kulipa kutokana na hali ngumu ya maisha katika familia yao.

Aliziomba taasisi nyingine kusaidia vijana wenye vikwazo vya kupata ada shuleni kwa madai kuwa walio wengine uwezo wao darasani ni mkubwa, hivyo wasaidiwe ili kutimiza malengo yao.



# Walimu wataka mazingira tulivu ya kufundishia uchaguzi mkuu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKUU wa shule za sekondari wameomba idara ya elimu sekondari kuwatengezea walimu mazingira mbadala ya ufundishaji kwa kipindi chote cha kampeni za uchaguzi mkuu ili kuepusha usumbufu unaoweza kuwapata wanafunzi.

Walisema kumekuwapo tatizo katika baadhi ya maeneo ya viwanja karibu na shule kutumiwa kufanywa mikutano mbalimbali ya kampeni na kupelekea kutokuepo umakini wakati wanapofundisha.

Walisema hayo katika mkutano wa mafunzo kwa walimu wakuu wa shule za sekondari juu ya kuwahamasisha wanafunzi kusoma kutokana ugonjwa wa virusi vya corona kupungua, na sasa ni kipindi cha uchaguzi mkuu.

Walisema kipindi cha uchaguzi kunakuwapo changamoto nyingi ambazo hupelekea wanafunzi kukosa muda mzuri wa kusoma kwa utulivu na hatimae lawama huwaangukia walimu.

Kutokana na hali hiyo, waliiomba wizara kuwaruhusu wanafunzi kutohudhuria shule katika siku za kampeni ambazo mikutano inafanyika katika maeneo ya viwanja vya shule ili kusaidia pia kuwaacha wanafunzi wakiwa salama wakiwa nyumbani kwao.

Akifungua mafunzo Mkurugenzi Idara ya Elimu Sekondari, Asiya Iddi Issa, aliwataka walimu wakuu kuhakikisha walimu wanatumia mbinu mbadala na ubunifu katika ufundishaji kwa sababu kumeonekana tatizo kwa baadhi ya wanafunzi kupunguza bidii ya kusoma kutokana na kufungwa shule kutokana na janga la Covid-19.

Alisema kuhamasisha wanafunzi kusoma kwa bidii kunahitaji kufundishwa kwa ubunifu wa hali ya juu ili kupata ufaulu wa kiwango cha juu wakati wa mitihani ya Taifa na ya majaribio.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Hamamni, Ali Rashid, lisema muda umefika kwa walimu kuwafundisha wanafunzi wao kwa vitendo hasa kuwapeleka maabara kwa masomo yanayostahiki badala ya kuwakaririsha.

Aidha, alisema katika kipindi cha uchaguzi mkuu muda wa masomo utapungua, hivyo ipo haja kwa walimu kutumia mbinu mbadala ili kuhakikisha wanafunzi wanazingatia masomo na kuacha kushiriki katika masuala ya siasa.

Akiwasilisha mada ya uchaguzi na elimu, ofisa kutoka Idara ya Elimu Sekondari, Haroub Ali Hamad, aliwataka walimu wakuu kuhakikisha wanawasimamia vyema walimu wao na wao wenyewe katika suala la kutohubiri siasa wanapokuwa shule badala yake kushughulikia suala la elimu.

Katika mafunzo hayo mada mbalimbali ziliwasilishwa ikiwamo wajibu wa mwalimu baada ya covid-19, walimu kuhakiki upatikanaji wa vifaa vya maabara na wajibu wa mwalimu mkuu kuelekea uchaguzi mkuu.



Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, akizungumza na wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU) katika viwanja vya Mapinduzi Square, Kisonge mjini Unguja. **PICHA NA RAHMA SULEIMAN**

## UVCCM yalaani kauli za wanasiasa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), umelaani vikali matamko ya baadhi ya viongozi wa siasa wanayoyatoa ambayo yamekuwa yakiashiria uvunjifu wa amani kuelekea uchaguzi mkuu Oktoba mwaka huu.

Naibu Katibu Mkuu wa UVCCM Zanzibar, Mussa Haji Mussa, aliyasema hayo,wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema hivi karibuni baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa wamekua wakitoa matamko yanayoashiria uvunjifu wa amani baada ya wagombea wao wa nafasi ya ubunge kuwekewa pingamizi.

Alisema kauli hizo zimekuwa zinakwenda kinyume cha maadili ya vyama vya siasa ambayo yametiwa saini na vyama vyote na kuridhiwa na tume ya uchagzui.

Aidha, alisema suala la wagombea kuwekewa pingamizi lipo kisheria kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi kifungu Namba 51 (1) cha sheria ya uchaguzi Namba nne ya mwaka 2008, ambapo mgombea yoyote wa chama anaweza kuwekewa pingamizi.

Naibu huyo alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama kuwachukulia hatua viongozi wanaotoa maneno ya uchochezi wakati wakizungumza na wafuasi wao.

Mussa alidai kuwa kauli hizo zinakwenda kinyume cha matamko ya vyama vya siasa ambalo limetiwa saini na vyama vyote na kuridhiwa na tume ya uchaguzi Zanzibar.

Aidha alisema kuwa UVCCM itahakikisha inapigania amani na utulivu kabla na baada ya uchaguzi.

# Vyuo vikuu waonyeshwa fursa ya ajira

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, amewataka wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu kusoma kozi ambazo zitawasaidia katika kujiajiri na kuajiri watu wengine.

Kauli hiyo aliitoa wakati akifungua siku maalum kwa wanafunzi wapya wanaotegemea kujiunga na Chuo Kikuu cha Zanzibar katika mnara wa kumbukumbu wa Mapinduzi Squere Michenzani Zanzibar. Alisema wanafunzi wengi wanapomaliza masomo ya elimu ya juu, wamekuwa wakitegemea sana ajira kutoka serikalini bila ya kufahamu kuwa serikali haina uwezo wa kuajiri watu wote.

Aidha, alisema umefika wakati kwa wanafunzi hao kuwa na upeo wa kuchagua na kuzingatia masomo ambayo yatawezesha kujiajiri wenyewe na kuajiri wengine.

Naibu Simai, alisema kuna fursa nyingi za ajira na soko kubwa hasa katika sekta ya utalii na sekta nyengine nchini ambazo zitawezesha vijana kujiajiri na kujikwamua na umasikini. Alieleza kuwa vijana wanapaswa kutambua kwamba kujiunga na chuo kikuu ni kujielekeza katika soko la ajira na mfumo mzima wa maisha kwa vijana, hivyo elimu ya juu ni muhimu kwa maendeleo katika sekta mbalimbali nchini.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikiweka mazingira mazuri na kutoa fursa mbalimbali za kusoma na kuanzisha vyuo vikuu nchini ikiwamo chuo kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) ili kuona vijana wanapata ujuzi wa kuisaidia nchi yao. Naye Naibu Katibu Mkuu Taaluma, Madina Mjaka Mwinyi, aliwataka wanafunzi kuitumia siku hiyo kupata maelezo ya kujiunga na chuo ili kupunguza changamoto mbalimbali katika uombaji.

Kwa upande wake, Msaidizi Naibu Makamo Mkuu wa Chuo hicho, Profesa Mohammed Makame Haji, alisema kumekuwa na matatizo mengi ya kujiunga na chuo katika miaka ya nyuma, hivyo wametumia siku hiyo kuwaeleza wahitimu ili kutokosa fursa ya kujiunga na chuo.

Alisema, chuo hicho kimekuja na kozi mbalimbali ambazo zimeangalia mahitaji ya nchi na hata katika soko la ajira la moja kwa moja.

Mwakilishi wa Benki of Afrika (BOA) tawi la Zanzibar, Linda Keyenja, alisema benki hiyo imeona umuhimu mkubwa wa kusaidia jamii kwa kuwapa fursa wanafunzi kwa huduma mbalimbali zinazotolewa na benki hiyo, ikiwamo kutoa mikopo kwa muda mfupi na akaunti za akiba kwa wanafunzi.

# Mshtakiwa ubakaji mtoto adai alipigiwa simu

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

MTUHUMIWA Abdulrahman Ubwa Daudi, mkazi wa Selemu Wete, anayekabiliwa na shtaka la kumbaka msichana wa 17 amedai kuwa, alipigiwa simu na msichana huyo na kumfuata Bopwe.

Alidai kuwa, yeye anafanya biashara ya kuuza mitumba ya nguo, hivyo kawaida yake hupigiwa simu na watu mbali mbali.

Mtuhumiwa huyo alidai kuwa msichana huyo anaishi Chasasa, ingawa alimfuata yeye Bopwe baada ya kumpigia simu, kwani alihisi ni wateja wake.

Alidai kuwa awali hakuwahi kumfahamu, ingawa alianza kujuana nae baada ya kumpigia simu hiyo na kumfuata.

"Alinipigia simu halafu akanifuata Bopwe wakati yeye anaishi Chasasa, sijambaka", alidai mtetezi huyo.

Pia aliiambia mahakama kuwa, anae shahidi ambae ni mama yake na atamfikisha mahakamani tarehe ijayo atakayopangiwa.

"Mama yupo Unguja anaumwa, hivyo akirudi nitakuja nae kwa sababu ndie shahidi wangu", alidai mtuhumiwa huyo.

Awali baada ya mtuhumiwa huyo kupanda kizimbani akisubiri taratibu za mahakama, ndipo mwendesha mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka, Juma Mussa Omar alipodai kuwa shauri hilo lipo kwa ajili ya utetezi.

Hakimu wa mahakama hiyo, Abdalla Yahya Shamhun, alikubaliana na upande wa mashitaka na ndipo alipomtaka mtuhumiwa huyo ajitetee ikiwa atakuwa tayari.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa, mtuhumiwa huyo alitenda makosa mawili ambapo kosa la kwanza alilitenda Oktoba 18, mwaka 2019, bila ya halali na bila ya ridhaa ya wazazi wake alimtorosha mtoto wa miaka 17 kutoka nyumbani kwao Chasasa na kumpeleka Bopwe.

Kufanya hivyo ni kosa kinyume na kifungu cha 113 (1) (a) cha Sheria namba 6 ya mwaka 2018, Sheria ya Zanzibar.

Kosa la pili kwa mtuhumiwa huyo anadaiwa alilitenda siku hiyo hiyo majira ya saa 06:00 mchana katika eneo la Bopwe Wilaya ya Wete, Mkoa wa kaskazini Pemba.

Ilidaiwa bila ya halali na bila ridhaa ya wazazi wake, alimbaka mtoto wa kike mwenye umri wa miaka17 mkaazi wa Chasasa Shehia ya Utaani, jambo ambalo ni kosa kisheria.

Kufanya hivyo ni kosa kisheria kinyume na kifungu cha 108 (1) (2) (e) na 109 (1) cha Sheria ya adhabu namba 6 ya mwaka 2018 sheria ya Zanzibar.

Kesi hiyo itarudi tena mahakamani Septemba 17, mwaka huu kwa ajili ya kusikilizwa shahidi wa upande wa mtuhumiwa.



Mafundi wa Kampuni ya Yapi Markezi wanaojenga Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR), wakiendelea na ujenzi wa daraja la reli hiyo katika eneo la Karume, Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wakulima wauza Mbaazi kwa mfumo wa stakabadhi ghalani

**Na Stevie Chindiye, TUNDURU**

JUMLA ya kilo 291,540 za Mbaazi zimeuzwa na wakulima wilayani Tunduru mkoani Ruvuma kupitia mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani katika mnada wa tatu uliofanyika katika msimu wa mwaka 2019/2020 .

Mnada huo ulifanyika katika viwanja vya Ofisi za chama cha ushirika cha Mlingoti Maghalibi, AMCOS jumla ya wanunuzi kutoka kampuni mbili walijitokeza na kutoa mbei tofauti na mnunuzi mmoja kati yao alishinda na kununua mbaazi hizo kwa bei ya Sh. 736 kwa kila kilo moja ya zao hilo.

Aidha, jumla ya Sh. 214,573,440:00 zilipatikana na zinatarajiwa kusambazwa kwa wakulima waliokubali kukusanya katika vyama vya msingi AMCOS na kuuza Mbaazi zao kupitia mfumo huo na kuongeza mzunguko wa fedha katika wilaya.

Alisema fedha hizo zitasambazwa kwa wakulima baada ya mshindi wa mnada huo kuingiza fedha kwenye akaunti ya chama kikuu na kukamilika kwa taratibu za makato ya kisheria ambayo ni wastani wa kati ya Sh. 84 hadi 99 kwa kilo moja iliyouzwa kupitia mfumo huo.

Bisani aliendelea kubainisha kuwa baada ya mauzo hayo mkulima hukatwa kiasi hicho kutokana na gharama za chama Kikuu (TAMCU) Sh. 15, Chama cha ushirika (AMCOS) Sh. 35 mchango wa elimu Sh. 2 na gharama za usafirishaji wa mazao ya mkulima kutoka Chama cha Msingi hadi ghala kuu la kuuzia mazao ni kati ya Sh. 47 hadi 70 kwa kila kilo moja ya mazao ya mkulima.

Awali, Kaimu ofisa Ushirika wa Wilaya ya Tunduru, Goerge Bisani, alisema fedha hizo zinatarajiwa kulipwa kupitia utaratibu wa kuwalipa wakulima walio kubali kuuza mbaazi zao kupitia mfumo huo baada ya wanunuzi hao kuingiza fedha katika vyama vya ushirika vya wakulima vilivyo kusanya mbaazi zao na kuwaingizia fedha zao kwenye akaunti zao za mbenki.

Wakizungumza kwa niaba ya Meneja wa TAMCU, Imani Kalembo na Yasini Masiano, waliwataka wakulima walioshirki katika mnada huo kuwa makini kusikiliza bei zinazo somwa kutoka kwenye Barua za wanunuzi walio omba kununua mazao yao ili waweze kuchagua bei kubwa kuliko zote.

Makamu Mwenyekiti wa TAMCU, Mussa Manjaule, pamoja na kuwapongeza wanunuzi walioshiriki na walioshinda na kununua mbaazi hizo kwa wakulima kufanya malipo kwa haraka ili kufanikisha malipo ya wakulima kwa wakati .

Aidha, aliwahamasisha kuendelea kukusanya mbaazi nyingi zaidi na kuleta mnadani tofauti na awali ambapo wengi wao wamekuwa wakivutiwa kuuza kwa wanunuzi holela.

Alisema wilaya imeanza vizuri msimu huo kwa kuuza mazao ya wakulima kwa bei mzuri na kwamba wanunuzi bado wanaendelea kuongeza bei katika minada ijayo, ili kuwashawishi wakulima wengi zaidi waendelee kukusanya mazao yao kwenye vyama vya msingi ili waweze kuuza kwa bei ambazo zitawawezesha kumudu kurejesha ghalama walizo tumia na kupata faida.

Alisema utaratibu wa kununua mazao katika maghala unamanufaa makubwa hata kwa wanunuzi wenyewe kwani unawapunguzia usumbufu na riski ya kupoteza fedha zao.

Takwimu zinaonyesha kuwa hadi mnada wa tatu tayari wakulima wameuza kilo 1,110,370 zilizo ingiza pato la Sh. 711,309,295:2 katika Wilaya ya Tunduru

# Wanakijiji wapewa jukumu kutunza maji

**Na Restuta Damian, KARAGWE**

KAMATI ya mazingira wilayani Karagwe mkoani Kagera kwa kushirikiana na uongozi wa Kijiji cha Nyakagoyagoye wametakiwa kutunza chanzo cha maji ikiwamo kuchangisha fedha.

Fedha hizo imeelezwa kuwa zitasaidia kwenye ununuzi wa dawa za kutibu maji hayo

Katibu Tawala wa Mkoa Kagera, Profesa Faustine Kamuzora, alisema hayo wakati akizungumza na viongozi wa kijiji, kamati ya maji wilaya, na viongozi wa shirika lisilo la kiserikali linalojihusisha na utoaji wa huduma za jamii na imani kiroho (World Vision) waliofika kukabidhi mradi wa maji katika Serikali ya mkoa huo.

Mradi huo umejengwa kwa ufadhili wa Ujerumani kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 400.

Profesa Kamuzora alisema, kama mazingira ya miundombinu ya maji yakiwekwa kwenye hali ya usafi unaozingatia matunzo bora, unaweza kuondoa magonjwa yanayotokana na matumbo hasa kwa watoto wadogo.

Alisema usimamizi utakaofanywa na kamati za mazingira uwe na ratiba ya kuchangisha wananchi fedha ambayo itakuwa ikinunua dawa za kutibia maji hayo ambayo yamekabidhiwa Serikali kwa ajili ya manufaa ya wananchi.

Aidha, alisema vituo vya afya na hospitali kwa asilimia kubwa zinapokea matatizo ya magonjwa ya upungufu wa maji kwa asilimia 70, ambayo yote hayo ni ukosefu na uhaba wa maji ya uhakika.

"Pia maji yana faida nyingi na sio kuondoa magonjwa ya tumbo na upungufu wa maji mwili pekee bali na kuanzisha bustani majumbani na kujipatia lishe bora ya watoto,"alisema Profesa Kamuzora.

Meneja mradi wa World vision Kanda ya Kagera, Juliana Charles, alisema mradi huo utahudumia wananchi ambao awali walikuwa walitumia muda mrefu kufuata maji vijiji jirani ambayo bado yalikuwa hayapo katika usalama.

Charles alisema kuwa baada ya kupatiwa taarifa na kamati ya maji kijiji hapo, shirika liliweza kufika eneo la chanzo na kufanya tathmini ya shughuli ya ujenzi utakaoweza kuzua mifugo isiweze kuingia ndani ya maji hayo kwa kuyazumgusha.

Mwenyekiti wa kijiji cha Nyakagoyagoye, Salmoni Mtilani, alisema kukamilika kwa ujenzi huo utaondoa watoto kutumia muda mwingi kutafuta maji na wakati mwingine kutokuhudhulia shuleni.

# Ekari 892 kujengwa kituo mafunzo ya reli

**Na Elizabeth Zaya**

CHUO Cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), kimetengewa zaidi ya ekari 892 Makao Makuu ya nchi Dodoma kwa ajili ya kuanzisha Kituo cha mafunzo ya usafirishaji na teknolojia ya reli.

Akizungumza baada ya Baraza la Chuo hicho kutembelea Shirika la Reli Tanzania (TRC), Mkuu wa Chuo, Prof. Zacharia Mganilwa, alisema Kituo hicho kitakuwa kikitoa mafunzo ya kitaalamu, kufanya utafiti na kutoa ushauri katika usafiri wa reli.

"Kituo hicho cha ubora kitajikita zaidi katika usafiri wa reli na utengenezaji wa vichwa vya treni pamoja na matengenezo mengine yahusuyo reli," Prof. Mganilwa alisema.

Alisema kuwa Chuo kinatarajia kuanza kutoa kozi ya wahandisi wa reli kwa lengo la kuiwezesha Tanzania kufikia uchumi wa juu ambapo mpaka sasa wameshaunda mitaala mbalimbali ili mwaka wa masomo 2020-2021 waweze kuanza masomo hayo.

"Kwa sasa Tanzania hatuna wataalamu wa kutosha katika taaluma ya mambo ya reli, sasa tunaelekea kuanza kuzalisha wataalaamu hapa hapa nchini ili wakizalishwa kwa wengi waweze kusimamia miundombinu ya usafirishaji wa reli."

Matarajio yetu baada ya kuanza kufundisha hao wataalamu kwa maana ya mafundi na wahandisi watapata fursa ya kuja kufanya mazoezi kwa vitendo na baadae kuajiriwa na shirika kwa manufaa ya Taifa letu" Mkuu wa Chuo," aliongeza.

Wajumbe hao walifurahishwa na kazi kubwa iliyofanywa na Serikali, huku wakilipongeza Shirika kwa kusimamia mradi mkubwa kwa kushirikiana na kampuni za ndani ya nchi na nje.

"Tunapozungumzia Tanzania kuingia katika uchumi wa kati maana yake ni Taifa liloendelea, umefanikiwa kuunganisha mikoa yote ya Tanzania bara kwa barabara za lami kinachofuta sasa ni kuunganisha mikoa yote kwa usafiri wa reli, katika miaka 10 ijayo tuna majiji sita," alisema na kuendelea:

Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, alielezea mchango unaoendelea kutolewa na NIT katika kutoa wataalamu mbalimbali nchini katika sekta ya usafirishaji pamoja na ushiriki wa Shirika la Reli kitaaluma katika kuandaa mitaala ya kufundishia wanafunzi, ambapo kimsingi imekuwa ni chachu ya kukuza sekta ya reli, lakini pia katika kujenga uhusiano wa karibu na wenye tija katika maendeleo ya Taifa kupitia usafirishaji na uchukuzi.

"Sisi kama Shirika kazi yetu ni kusafirisha na wao kama Chuo ni kutoa wataalamu ambao watakuja kusimamia uendeshaji wa reli, kwa hiyo hiki ni chuo ambacho ni muhimu sana kwa Shirika," alisema Kadogosa.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa (kulia), akifafanua jambo alipotembelewa na viongozi wa Baraza la Uongozi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) makao makuu jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Shia waadhimisha kifo cha mjukuu Mtume Muhammad kwa maandamano

**Na Mwandishi Wetu**

JUMUIYA ya Khoja Shia Ithnasheri kwa kushirikiana na madhebu yote ya Shia, imefanya maandamano ya amani katika kukumbuka kifo cha mjukuu wa Mtume Muhammad, (SAAW), Imam Hussain.

Maandamano hayo ni muendelezo wa kuadhimisha mwezi mtukufu wa Muharram sambamba na kumbumbuku ya kifo cha mjukuu wa Mtume Muhammed (SAWW), Imam Hussain.

Tukio hilo limefanyika wiki moja baada kupitia programu yake ya "Hussain Blood Drive" kufanikisha uchangiaji damu kwa kushirikiana na Mpango wa Taifa wa Damu Salama na Hospitali ya Ebrahim Haji.

Akizungumza katika zoezi hilo, mmoja wa viongozi wa madhehebu ya Shia ambae pia ni kiongozi Mkuu wa Chuo cha Dini ya Kiislam kilichopo Kigogo jijini Dar es Salaam, Sheikh. Hemed Jalala, alisema: "Matembezi haya ya amani ni sehemu ya kumbukumbu ya kifo cha mjukuu wa Mtume Muhammed (SAWW), Imam Hussain, ambae aliuawa zaidi ya miaka 1,300 iliyopita huku akiamini katika uhuru na mshikamano ambao hata sisi leo tunauhitaji kwa ajili ya maendeleo na mafanikio ya nchi yetu."

Sheikh Jalala alisema pamoja na uhuru na mshikamano, Imam Hussain aliamini katika kutunza amani na utulivu jambo ambalo Watanzania wanalihitaji sana hususan kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi ilikuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kubaki kuwa kisiwa cha amani na utulivu.

"Lengo la kutoka kwa matembezi haya kwa ajili ya Imam Hussain (as), nikutaka kupaza sauti kwamba amani, utulivu na upendo ni mambo muhimu ambayo yanapaswa kuenziwa na kutazamwa kwa umakini," alisema Sheikh Jalala.

Maandamano hayo ya yamefanyika siku ya Ashura ambayo ni siku ya kumi ya mwezi wa Muharram. Zaidi ya Miaka 1,300 iliopita, Katika siku hii ya Ashura mjukuu wa Mtume yaani Imam Hussain (as) aliuawa katika tambarare za mji wa Karbala, Iraq.

Siku hii huadhimishwa kila mwaka, ili kutunza thamani ya mafundisho ya Imam Hussain (as) ambae alisimamia katika kuamrisha mema na kukataza mabaya. "Amr bil Marouf na Nahyanil Munkar"

Pamoja na maandamano hayo, Jumuiya ya Khoja Shia Ithnasheri imekuwa ikifanya matukio yanayolenga kusaidia jamii kumuenzi mjukuu huyo wa Mtume. Mambo hayo ni kuchangia damu huku pia ikiratajia kufanya uchunguzi na upasuaji wa mtoto

## SPC yakumbusha waandishi maadili

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MWENYEKITI wa chama cha waandishi wa habari mkoani Shinyanga (SPC), Greyson Kakuru, amewataka waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari mkoani hapa kuhakikisha wanafuata maadili ya habari kwa kipindi hiki cha uchaguzi ili kuepuka kuingia kwenye migogoro na vyama vya kisiasa.

Kakuru alitoa kauli hiyo jana wakati alipoitisha kikao cha dharura kwa waandishi wa habari wa wilayani Kahama, mkoani Shinyanga na kutoa maagizo ya uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Alimtaka kila mwandishi kufuata maadili na miiko ya taaluma ya uandishi wa habari.

Alisema kuwa kwenye kipindi cha uchaguzi waandishi wengi wa habari wanaingia kwenye migogoro na vyama vya kisiasa baada ya kupata habari ya upande mmoja na kuirusha hewani au kuichapisha kwenye magazeti bila kujua anatakiwa kuweka uwiano na upande wa pili.

"Ndugu zangu, tuepuke kuingia kwenye migogoro ambayo tunaweza kuepuka, tukipata habari kupitia kwenye vyama vyetu vya kisiasa tuhakikisha tunapata uwiano (balance) upande wa pili ili mwisho wa siku tuwe wasafi na tusiingie kwenye migogoro," alisema Kakuru.

Aliongeza: "Kwenye mikutano ya hadhara wanasiasa huwa wanatupiana vijembe na tuhuma mbalimbali kwa vyama flani, tuhakikishe tunapata ufafanuzi wa uhakika kwa chama kilichotupiwa tuhuma na sio kuichukua kama ilivyo na kuiweka kwenye chombo vyetu vya habari."

Kwa upande wa Katibu wa chama hicho Ali Lityawi, alisema kuwa kila mwandishi anatakiwa kuwa makini katika kipindi hiki cha uchaguzi na kuepuka kuonekana kama wanatumiwa na chama fulani kwa maslahi ya chama hicho na sio badala ya maslahi ya Watanzania.

Pia alisema waandishi wanatakiwa kuhakikisha wanaweka mbele ushawishi kwa viongozi wa kisiasa kuchukua idadi kubwa ya waandishi ili kupanua wigo wa kuripotiwa habari zao.



# MATIC:
## MAN UNITED INAWEZA KUSHINDA TAJI LA EPL

**MANCHESTER, England**

NYOTA wa Manchester United, Nemanja Matic, anamini Mashetani wekundu hao wanaweza kushinda Ligi Kuu England, akionya hakutakuwa na msamaha kwa msimu wa 2020-21.

United ilifurahia kucheza mechi 14 mfululizo bila kufungwa na kumaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England msimu uliopita, nyuma ya mabingwa Liverpool na Manchester City.

Kikosi hicho cha Ole Gunnar Solskjaer, United, ambaye alimaliza kwenye nusu fainali ya kombe la Ligi ya Europa, FA na EFL mwaka 2019-20, pia ilifuzu kwa ligi ya mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2017-18.

United ilimaliza ikipitwa pointi 33 na wapinzani wao Liverpool, lakini kiungo mkongwe Matic anaamini wana nafasi kubwa kuelekea msimu huo mpya.

"Kuanzia msimu ujao hakutakuwa na msamaha," alisema Matic akiiambia UTD Podcast.

"Tunakwenda na kila kitu. Tunatakiwa kupambana kwa ajili la taji kwa sababu mwaka huu tulipoteza baadhi ya pointi kirahisi zaidi.

"Tuliwaruhusu Liverpool kushinda (taji), sijui, mechi 10 kabla ya msimu kumalizika. Walishinda ligi, hivyo hatuwezi kuruhusu hilo. Tunahitaji kupambana hadi mwisho. Tunatakiwa kucheza kwa kujiamini zaidi."

## SOUTHGATE AKUNWA HENDERSON KUBAKI MAN UTD

**LONDON, England**

KOCHA wa England, Gareth Southgate, ameunga mkopo uamuzi wa Dean Henderson kubakia Manchester United na kutoa changamoto kwa David de Gea katika nafasi ya golikipa namba moja.

Henderson amerudi pale Old Trafford bada ya kuwa na kiwango cha kuvutia wakati akicheza kwa mkopo kule Sheffield United msimu uliopita, akiwa amesaini mkataba mpya wa miaka mitano na Manchester.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ambaye amejumuishwa kwenye kikosi cha Southgate cha England kwa ajili ya mechi za Ligi ya Mataifa ya Uefa dhidi ya Iceland na Denmark, yupo kwenye nafasi ya kushindana na nyota namba moja wa United, De Gea.

Southgate anahisi ni muda muafaka kwa Henderson kujipa changamoto yeye mwenyewe baada ya misimu miwili ya mafanikio pale Sheffield United.

"Nafikiri ni nafasi yake kwa sasa," amesema Southgate akiwaambia waandishi wa habari.

"Bilashaka, angeweza kuchukua msimu mwingie nje na kupata uzoefu kwenye Ligi Kuu, lakini kwa umri wake huwezi tu kufikiria kuhusu hiyo.

"Anajenga kipaji chake na pale kuna nafasi kubwa ya kutengeneza changamoto kwa ajili yake akiwa na jezi ya Manchester United.

"Nafikiri kwa umri wake ni uamuzi sahihi sasa kupewa nafasi ya kucheza mechi pale United msimu ujao."

## KLOPP: MINAMINO ATAFANYA MAKUBWA LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesisitiza Takumi Minamino anaweza kuwa na mchango mkubwa baada ya kufunga bao lake la kwanza kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii.

Mshindi wa taji la FA, Arsenal, iliwafunga Liverpool kwa penalti 5-4 baada ya sare ya 1-1 kwenye mchezo wa Jumamosi katika uwanja wa Wembley ukiwa ndio unafungua pazia la msimu mpya wa Ligi Kuu ya England.

Minamino bao lake hilo la kwanza kwa Liverpool lilifuta lile la Pierre-Emerick Aubameyang alilofunga dakika ya 12 mjini London, ambapo penalti ndio ililazimika kuamua bingwa.

Star wa Japan, Minamino, alijiunga na Liverpool kutoka Salzburg Januari, lakini hakuweza kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara wakati wekundu hao wakitwaa taji lao la kwanza la Ligi Kuu kwa kipindi cha miaka 30.

Lakini baada ya Minamino kufungua kaunti yake ya mabao kwa Liverpool, Klopp aliwaambia waandishi wa habari:

"Lilikuwa jambo kubwa kwake na kwetu kwa sababu kilikuwa kitu pekee alichokikosa tangu ajiunge na sisi.

"Hakufunga bao hapo kabla, lakini kulikuwa na nyakati ambazo alikaribia kufunga. Hili limemsaidia. Kwa sasa nafikira atakuwa na hali nzuri na anajiona mmoja wa wachezaji muhimu kwenye kikosi."

Klopp aliongeza: "Anaweza kuwa na mchango mkubwa, ndio maana tulimsajili. Hilo ni jambo rahisi ninaloweza kusema."






# ARSENAL INASTAHILI KUWA NNE BORA EPL, UEFA – TIERNEY

**LONDON, England**

MLINZI wa pembeni wa Arsenal, Kieran Tierney amesema klabu hiyo inastahili kuwa kwenye nne bora na kufuzu kucheza Ligi ya mabingwa Ulaya baada ya kushinda Ngao ya Jamii dhidi ya Liverpool.

Pierre-Emerick Aubameyang alifunga penalti ya ushindi baada ya Arsenal kuibeba Ngao ya Jamii kwa ushindi wa changamoto ya mikwaju ya penalti 5-4 dhidi ya Liverpool katika uwanja wa Wembley, Jumamosi.

Takumi Minamino alifunga bao lake la kwanza kwa Liverpool ambalo lilifuta lile la Aubameyang alilofunga mapema dakika ya 12 mjini London, ambako kocha wa Arsenal, Mikel Arteta ameonekana kukifanyia mapinduzi makubwa kikosi hicho.

Arsenal ilimaliza nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi msimu uliopita, ikifuzu kucheza Ligi ya Europa kwa mara ya nne mfululizo, lakini Tierney amesisitiza kujiamini hapo kwenye dimba la Emirates.

"Ari ni moja ya kitu muhimu kwenye vyumba vya kubadilishia nguo, imani na hamasa tuliyonayo itatufanya tujenge timu vizuri zaidi," alisema.

"Tunaangalia na kuendelea kuijenga timu yetu kwa njia hii.

"Fikra hizo zinakuja kutoka kwa kocha na benchi lote. Tunaendelea kutoka kile tulichokifanya msimu uliopita.

"Tumeonekana kurudi ndani ya wiki chache zilizopita na tumerudi ili kuendelea pale tulipoishia. Hatujawa na kipindi kirefu cha mapumziko.

"Kuja kwenye mchezo kama huu ni sawa na kuanza kuamini zaidi na zaidi na kufikiria kwamba, tuna imani na molari.


"Mikel alitupa hamasa tangu siku ya kwanza, safu yetu ya ulinzi imeimarika na imepitia kipindi cha mpito.

"Na hicho ndio tunachokifanya kila siku tukiwa kwenye mazoezi na tunaangalia video. Hii haijaja tu kwa bahati. Ni sababu ya kujituma.

"Mashabiki na klabu wanastahili kuwa kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya. Wanastahili kuwa kwenye nne bora ya Ligi Kuu na tunataka kufanya kadili tunavyoweza na kuendelea kupigana katika kila mchezo utakaokuja mbele yetu mwaka huu."

Arsenal itaanza kampeni yake ya Ligi Kuu kwa msimu wa 2020-21 dhidi ya timu iliyopanda daraja, Fulham Septemba 11, mwaka huu.

## MESSI ATAKWENDA MAN CITY – KOCHA



**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi anatakiwa kuondoka Barcelona kwenda kujiunga na Pep Guardiola pale Manchester City, amesema kocha msaidizi wa zamani pale Camp Nou, Juan Carlos Unzue.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, Messi aliushitua ulimwengu wa soka kwa kupeleka maombi ya kutaka kuondoka Barca wiki iliyopita.

City wanaonekana kama ndio wenye nafasi kubwa zaidi ya kuipata saini yake, huku Messi akiripotiwa kumpigia Guardiola - ambaye alikuwa kocha mkuu wa Barcelona kati ya mwaka 2008 na 2012 wakati Messi alipokuwa akitajwa kuwa mchezaji bora zaidi kuwahi kutokea kwenye sayari hii.

Unzue, ambaye alikuwa kocha msaidizi wa Guardiola kwa upande wa magolikipa pale Barca kabla ya kuwa msaidizi wa Luis Enrique kati ya mwaka 2014 na 2017, ana matumaini kutafikiwa suluhisho kati ya Messi na Manchester.

"Kwa upande mmoja, kama anaondoka Barcelona, ningependa aende kwa mtu ambaye alipata nae mafanikio makubwa," amesema akiiambia Stats Perform News.

"Matumaini yangu atakwenda Manchester City; hili nalisema kwa uwazi kabisa. Nina uhakika uamuzi wake utakuwa magumu sana.

"Pia nina uhakika anakumbuka uhusiano wake mzuri na Pep kwa sababu amekua pembeni yake."



## DEPAY: NAOTA KUCHEZA KLABU KUBWA

**LYON, Ufaransa**

NYOTA wa Lyon, Memphis Depay, amekubali kwamba "anaziota klabu kubwa tu" huku akihusishwa na uhamisho wa kwenda Barcelona.

Depay mwenye umri wa miaka 26, amekuwa akihusishwa na mpango wa kwenda kwa miamba hao wa LaLiga, ambako kocha wake wa zamani wa Uholanzi, Ronald Koeman amechukua mikoba pale.

Straika huyo alifunga mabao matatu 'hat-trick' wakati Lyon walipowafumua Dijon 4-1 kwenye mchezo wa ufunguzi wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Ijumaa.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Depay amesema alikuwa bado hajazungumza na Koeman, lakini alikubali alikuwa anaota kujiunga na klabu kubwa, huku Lionel Messi akitajwa kuondoka Barcelona.


"Kwa uhakika akili yangu ipo hapa Lyon. Nina furaha kwamba nimerudi, sijazungumza na Koeman bado," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Unajua amekuwa akihusishwa na kupona kwangu, alikuja Rama kuniona mimi, wakati nilipokuwa ninajifua nchini Uholanzi, alikuja kuniona hivyo nina uhusiano nae mzuri tu.

"Kwa sasa ni kocha mkuu wa Barcelona, na binafsi nimejikita zaidi Lyon kwa sababu ndio nipo hapa kwa sasa.

"Naweza kuota kwa klabu kubwa na tutaona nini kitatokea, lakini kwa wakati huu mimi ni mchezaji hapa na nina majukumu makubwa."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# LEWANDOWSKI: MKATABA HUU SIO WA MWISHO

●●●Kitu cha kwanza, mkataba wangu wa sasa hautakuwa wa mwisho, kwani malengo yangu ni kucheza kwenye daraja la juu baada ya...

**MUNICH, Ujerumani**

ROBERT Lewandowski hana mpango wa kumaliza kipindi chake cha uchezaji, akisisitiza ana kila kitu katika malengo yake ya kucheza katika daraja la juu kabla ya mkataba wake wa sasa kumalizika.

Lewandowski amefunga mabao 55 kwenye mashindano yote ya klabu msimu wa 2019-20, wakati Bayern Munich ikibeba taji la Bundesliga, DFB-Pokal na Ligi ya mabingwa Ulaya.

Nyota huyo wa kimataifa wa Poland alitimiza umri wa miaka 32 Agosti na mkataba wake wa sasa na Bayern unamalizika mwaka 2023, lakini malengo yake ni kuendelea kucheza baada ya hapo.

"Kitu cha kwanza, mkataba wangu wa sasa hautakuwa wa mwisho. Malengo yangu ni kucheza kwenye daraja la juu bada ya mwaka 2023," amesema Lewandowski akiiambia Onet na Przeglad Sportowy.

"Sifikiri nini nitakachofanya baadae. Sina hofu kuhusu afya yangu na ufiti wangu, lakini nina matumaini kwamba nitakuwa vyema kiakili na kuendelea kucheza kwa kiwango cha juu. "Wakati nitakapomaliza kucheza, kutakuwa na machaguo mengi, lakini sina mipango maalumu. Itategemea na hisia zitakavyoniambia."

Lewandowski alifika fainali ya Ligi ya mabingwa na Borussia Dortmund mwaka 2013, lakini hakuweza kulibeba taji hilo hadi alipokisaidia kikosi cha kocha, Hansi Flick kuifunga Paris Saint-Germain 1-0 mjini Lisbon kwenye fainali.

## KWA UFUPI

**BARCA WATARAJIA MESSI KUTUA MAN CITY**

MAOFISA wakuu wa Barcelona, wanatarajia kiungo wa Argentina, Lionel Messi, mwenye umri wa miaka 33, atajiunga na Manchester City. ***(Sunday Telegraph)***

**MAN CITY WAMTARAJIA MESSI**

KLABU ya Manchester City ina matumaini ya kumsajili Lionel Messi kwa kiasi kikubwa cha fedha, pamoja na kumpa mkataba mpya kocha, Pep Guardiola. ***(Sunday Mirror)***

**RODRIGUEZ HUYO EVERTON**

MCHEZAJI wa kimataifa wa Colombia, James Rodriguez mwenye umri wa miaka 29, atafanyiwa vipimo vya afya wiki ijayo pale Everton tayari kujiunga kwa mkopo wa muda mrefu kutoka Real Madrid. ***(Talksport)***

**AURIER AKATAA KWENDA WOLVES**

MLINZI wa Tottenham Hotspur, Serge Aurier raia wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 27, amekataa uhamisho wa kwenza Wolves kama sehemu ya dili la kumsajili Matt Doherty mwenye umri wa miaka 28 raia wa Ireland. ***(Daily Star Sunday)***

**INTER YAMUWANIA NDOMBELE**

INTER Milan imeiambia Tottenham Hotspur ina nia ya kumsajili, Tanguy Ndombele, lakini wanataka Spurs kupunguza bei yao ya pauni milioni 55 kwa kiungo huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 23. ***(Sunday Express)***

**VAN DE BEEK AISUBIRIA BARCELONA**

KIUNGO wa Ajax na Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 23, anasubiri kuona kama Barcelona watatoa ofa kwake kabla ya kufikiria kwenda Manchester United au Tottenham. ***(Sport)***

**OFA YA BRUYNE YASUBIRISHWA**

OFA mpya ya Manchester City kwa Kevin de Bruyne ya kumlipa mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki, imesubirishwa baada ya wakala wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 raia wa Ubelgiji kukamatwa na askari nchini humo. ***(Sunday Mirror)***

**VILLA WATAKA KURUDISHA ABRAHAM**

ASTON Villa inataka kumrudisha nyota wa Chelsea, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 22 pale Villa Park, baada ya kuwa na msimu wenye mafanikio wa 2018-19, lakini straika huyo wa England anataka kupigania nafasi yake pale Stamford Bridge. ***(Mail)***

**MARTINEZ AWANIWA ASTON VILLA**

ASTON Villa pia inaandaa ofa ya pauni milioni 10 kwa golikipa wa Arsenal, Emi Martinez mwenye umri wa miaka 27 raia wa Argentina. ***(Independent on Sunday)***

**HOLDING AWINDWA NEWCASTLE**

NEWCASTLE United imeonesha nia ya kutaka kumsajili mlinzi wa Arsenal, Rob Holding mwenye umri wa miaka 24, kwa mkopo wa muda mrefu. ***(The Athletic)***

**KEAN KUONGEZA MKATABA EVERTON**

MLINZI wa Everton na England, Michael Keane mwenye umri wa miaka 27, amekubaliana maslahi binafsi ya kusaini mkataba mpya hapo Goodison Park. ***(Football Insider)***



HABARI MICHEZO

# SOGNE WA YANGA KUTUA LEO NCHINI

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI Mpya wa Yanga, Yacouba Sogne, anatarajiwa kutua nchini leo kujiunga rasmi na kikosi hicho kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania bara.

Yacouba ni kati ya washambuliaji wa Yanga waliosajiliwa akitokea Asante Kotoko ya Ghana mara baada ya mkataba wake kumalizika na kujiunga na timu hiyo, kama mchezaji huru.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mjumbe wa Kamati ya Usajili ya Yanga, Injinia Hersi Said aliwaondoa hofu mashabiki juu ya ujio ya mshambuliaji huyo kwamba atatua nchini leo kwa ajili ya kujiunga rasmi na kikosi cha Yanga.

Alisema nyota huyo alitakiwa kuwasili katikati ya wiki iliyopita, lakini sasa atatua leo akitokea nyumbani kwao nchi Burkina Faso.

"Awali alitakiwa kufika nchini Alhamisi, lakini ndege aliyotakiwa kuja nayo Yacouba ilizuiliwa kutua nchini, sasa nyota huyo tunatarajia kutua nchini leo na kujiunga na kikosi tayari kuanza majukumu yake," alisema Hersi.

Alisema mshambuliaji huyo mara baada ya kutua nchini, haraka ataungana na na wachezaji kwenye kambi kwa ajili ya kuanza mazoezi ya pamoja kujiandaa na msimu mpya wa ligi.

Alisema msimu huu wamekuwa makini katika suala la usajili hasa kuzingatia mahitaji ya timu yako na mapendekezo ya benchi la ufundi.

"Tumesuka upya kikosi chetu, lakini pia benchi la ufundi nao lina mabadiliko hii ni kuhakikisha kwamba msimu wa 2020/21 tunafanya vizuri na kufikia malengo yetu ya kutwaa ubingwa," alisema Hersi.

Yanga itafungua dimba la Ligi Kuu Tanzania Bara, Septemba 6 wakiwa nyumbani dhidi ya Prisons kwenye uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam.




Naibu Waziri wa Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Anthony Mavunde (wa pili kulia), akiwa na Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla (kulia), wakiwapungia mashabiki wa Yanga waliojikeza jana kwenye kilele cha Siku ya Mwananchi katika Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA NA MTANDAO**

# Azam yajiweka mguu sawa Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC, umesema timu yao imejiandaa vizuri na ipo tayari kwa ajili ya kutoa ushindani kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuanza Septemba 6, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Aristica Cioaba, alisema maandalizi yanaendelea vizuri na ana imani kikosi chake kitampa mafanikio makubwa yanayotarajia katika Ligi hiyo.

Alisema ameridhishwa na usajili uliofanywa kwani umefuata vigezo vya ripoti aliyotoa kwa uongozi kwa wachezaji ambao anawahitaji na kusaidia kufika malengo.

"Tunaendelea mazoezi na programu, tumejiandaa vizuri kuhakikisha tunapata matokeo mazuri katika michezo yetu yote ya Ligi," alisema kocha huyo.

Alisema anaridhishwa na viwango vya wachezaji wao wote, wakiwemo wapya ambao wamefanikiwa kuingia katika mfumo wake wa haraka na kupata matumaini ya kufanya vizuri katika mechi zake.

Kocha huyo alisema kutoka na matokeo ya mechi za kirafiki na kiwango cha wachezaji wake wanampa imani ya kufanya vizuri na kuleta ushindani katika michezo yao ya Ligi hiyo.

Azam wataanzia nyumbani kuwakaribisha Polisi mchezo utakaopigwa Septemba 6, mwaka huu, Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi.

## Ihefu yahamia Sokoine kupisha ujenzi

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Ihefu imesema kuwa, mechi zake tatu za mwanzo itacheza kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya kupisha matengenezo kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Highland Estate mjini Mbarali.

Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Fredy Chalamila amesema kuwa hawatotumia uwanja huo kwenye mechi zao tatu za mwanzo, kwani hivi sasa uwanja wao uko kwenye matengenezo ambayo yatachukua mwezi mmoja.

"Tuna mechi ya kwanza tarehe sita dhidi ya Simba, halafu tutacheza na Mtibwa Sugar, baada ya yapo tutacheza na Ruvu Shooting. Zote hizo tutacheza kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, baada ya hapo tutakwenda Kanda ya Ziwa na tukishamaliza huko nadhani kila kitu kitakuwa sawa, tutaanza kuutumia uwanja wetu wa nyumbani," alisema Katibu huyo.

Chalamila alisema kuwa matengenezo yaliyopo ni ujenzi wa ukuta, lakini pia marekebisho kwenye jukwaa. "Tumeongea na mkandarasi, ametuambia kuwa ujezi utakamilika baada ya mwezi mmoja," alisema.

Ihefu, timu kutoka Mbarali mkoani Mbeya, imepanda daraja msimu huu na inatarajiwa kuanza kucheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza, huku ikipangwa kucheza na Mabingwa Watetezi Simba kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya.

Timu hiyo iliingia Ligi Kuu kupitia mechi ya mchujo, ikicheza dhidi ya Mbao FC na kushinda mabao 3-1 nyumbani, huku ikifungwa mabao 4-2 kwenye mechi ya marudiano na kufanikiwa kutinga Ligi Kuu kwa bao la ugenini.

## Alliance FC yazidi kubomolewa

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuteremka daraja, hali imezidi kuwa mbaya kwa Alliance FC ya Mwanza kwa kuzidi kuchukuliwa wachezaji wake, baada ya beki wao wa kutegemewa Luseke Kiggi kujiunga na Mtibwa Sugar.

Mtandao rasmi wa klabu ya Mtibwa Sugar umechapisha picha ya mchezaji huyo aliyepewa jezi ya klabu hiyo na kuandika kuwa amesajiliwa kwa mkataba wa miaka mitatu.

"Tumefanikiwa kuinasa saini ya beki wa kati Jofrey Luseke Kiggi, akitokea Alliance ya Mwanza. Tumeingia mkataba wa miaka mitatu na beki huyo hodari." Ilimaliza taarifa hiyo kwenye mtandao wa klabu hiyo.

Huu ni muendelezo wa Alliance kuondokewa na wachezaji wake muhimu baada ya kushuka daraja.

Wengine walioondoka ni beki wa kulia Israel Patrick aliyejiunga na KMC, Martin Kiggi aliyejiunga pia na KMC, wengine ni Wema Sadoki na Michael Chinedu ambao wote wamejiunga na Ihefu FC.

Alliance ilishuka moja kwa moja baada ya kumaliza ligi ikishika nafasi ya 17, ikiwa na pointi 45.

# Michezo

Jumatatu Agosti 31, 2020

Nipashe



HABARI UK 22

## LEWANDOWSKI: MKATABA HUU SIO WA MWISHO



Wachezaji wa Yanga wakiwa katika picha ya pamoja wakati wakitambulishwa kwa mashabiki wao, wakati wa kilele cha Siku ya Mwananchi katika Uwanja wa Benjamini Mkapa jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA NA MTANDAO**

# MORRISON AANZA KULIPA SIMBA IKIANZA NA TAJI

●●●Kilichobaki kwake ni chenji tu, awa mwiba mkali wakifungua tena msimu mpya kwa taji kama...

**Na Isaac Kijoti, ARUSHA**

USAJILI wa winga Mghana Bernard Morrison umeanza kulipa na kilichobaki ni kama kurejesha chenji tu kwa mabingwa wa Ligi Kuu Bara na Kombe la FA, Simba, baada ya jana kuibebesha Ngao ya Jamii.

Morrison aliibebesha Simba taji hilo baada ya kufunga bao moja na kuzalisha penalti iliyozamishwa nyavuni na John Bocco wakati wakishinda 2-0 dhidi ya Namungo FC kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Kwa kubeba Ngao hiyo ya Jamii ambayo ni maalumu kwa kukaribisha msimu mpya wa ligi, Simba itakuwa imeanza tena msimu kwa taji kama iliyokuwa msimu uliopita.

Mchezo huo ulionekana kuwa wa upande mmoja ambapo Simba ilitawala kipindi chote cha kwanza na cha pili kwa mpira kuchezwa zaidi katika lango la Namungo.

Kama Hassan Dilunga angekuwa makini katika dakika ya nne tu angeweza kuipatia Simba bao la kuongoza, lakini Kipa wa Namungo alikuwa makini na kudaka shuti lake.

Claotus Chama alionana vema na Bocco kabla ya pasi kumfikia Morrison aliyejaa nao ndani ya 18 na kuchezewa madhambi yaliyozaa penalti ambayo ilizamishwa kimyani na Bocco dakika ya saba.

Shambulio pekee la hatari lililofanywa na Namungo lilikuwa dakika ya 17 baada Sixtus Sabilo akiwa wingi ya kushoto kumpasia Stephen Sey, lakini alipiga shuti hafifu lililoishia mikononi mwa Kipa Aishi Manula.

Kipindi cha pili kilianza kwa Namungo kumuingiza Shiza Kichuya ambaye aliongeza uhai katika safu ya ushambuliaji iliyokuwa ikiongozwa na Bigrimana Blaise.

Hata hivyo, hawakuweza kufurukuta katika safu ya ulinzi ya Simba iliyokuwa chini ya ulinzi mkali wa Mkenya Joash Onyango na Kennedy Juma.

Bao la pili lilipatikana dakika ya 60 kwa mpira mrefu uliopokelewa na Mzamiru Yassin na kisha kumpenyezea pasi Claotus Chama aliyetoa pande kwa Morrison ambaye aliachia shuti kali lililojaa wavuni.

Baada ya bao hilo Kocha wa Simba, Sven Vandenbroeck alimtoa Morrison na kumuingiza Rally Bwalya, ambaye alizidi kulitia hatarini lango la Namungo.

Simba ilifanya tena mabadiliko dakika ya 79 kwa kumtoa Hassan Dilunga na kumuingiza beki Ibrahimu Ame huku John Bocco akimpisha Meddie Kagere.

Hiyo ni mara ya tatu Simba inashinda dhidi ya Namumgo katika mechi nne timu hizo zilizokutana hadi sasa.

Mara ya kwanza timu hizo kukutana ilikuwa Januari 29, mwaka huu kwenye mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Bara mechi ikipigwa Uwanja wa Taifa/Mkapa na 'Wekundu wa Msimbazi' hao kushinda 3-2.

Mabao katika mechi hiyo yalifungwa na Francis Kahata dakika ya 21, Hassan Dilunga (dk. 38) na Meddie Kagere (dk. 88), wakati yale ya Namungo yakizamishwa kimyani na Bigirimana Blaise (dk. 35) na Lucas Kikoti dakika ya 71.

Mzunguko wa pili katika mechi ya ligi hiyo iliyopigwa Julai 20, mwaka huu Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi, timu hizo zilitoka sare tasa.

Mchezo wa tatu kuzikutanisha timu hizo ilikuwa kwenye fainali ya Kombe la FA iliyopigwa Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga Agosti 2, mwaka huu na Simba kutwaa kombe hilo kwa ushindi wa mabao 2-1.

Mabao ya Simba yalifungwa na Luis Miquissone dakika ya 28 na John Bocco (dk. 39) huku la kufutia machozi la Namungo likifungwa na Edward Manyama dakika ya 56.

Simba itapeperusha bendera ya nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Namungo ikibeba jukumu hilo kwa upande wa Kombe la Shirikisho Afrika.

# YANGA YAFUNIKA SIKU YA MWANANCHI

**Na Adam Fungamwango**

MAELFU ya wanachama na mashabiki wa Yanga jana walifurika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kushuhudia tamasha la Wiki ya Mwananchi.

Asubuhi na mapema mitaa ya Dar es Salaama ilipambwa na ngoma, bendera, khanga na magari yaliyokuwa yakielekea kwenye uwanja huo na kuujaza, kuadhimisha tamasha hilo la kila mwaka, ambalo huanza kwa kufanya shughuli za kijamii kwa muda wa wiki nzima, kabla ya kuhitimishwa na utambulisho wa wachezaji watakaoichezea klabu hiyo kwa msimu mzima.

Yanga ambayo jana ilicheza dhidi ya Aigle Noir kutoka nchini Burundi, ilitambulisha wachezaji wote wa zamani na wapya, wakiwamo wale waliopokelewa kwa mbwembwe Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere.

Wachezaji waliopolekewa ni kama Mukoko Tonombe, Tuisila Kisinda, kutoka AS Vita ya nchini Congo DR, na Carlos Stenio Fernandes Giumaraes do Carmo maarufu kama Carlinho kutoka klabu ya Interclube ya Angola.

Ilikuwa ni saa 10:00 jioni wakati wachezaji wa Yanga walipojitokeza wakiwa wamevaa suti za bluu iliyokolea na kusababisha mayowe kutoka kwa umati uliofurika uwanjani hapo.

Wachezaji wa zamani wa timu hiyo kwa nyakati tofauti, Abeid Mziba na Sunday Manara wamesema kuwa wamefurahishwa na mashabiki wengi kujitokeza, lakini pia wakiwa na imani na kikosi kilichosajiliwa msimu huu, ili mradi kuwe na mshikamano kwa wachezaji wenyewe.

Yanga inaonekana kujipanga upya msimu huu, baada ya kufanya usajili mkubwa, huku ikiacha jumla ya wachezaji wapatao 16 wa ndani na nje ya nchi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >